# *KUISHINDANIA ILE IMANI*

Asante, Ndugu Arganbright. Habari za jioni, marafiki. Huo ulikuwa utambulisho mzuri kabisa, sivyo, "Rais wa Marekani"? Tuna furaha kuwa hapa usiku wa leo, katika ukumbi huu hapa Georgetown, Indiana.

2 Nilipokuwa nikishuka barabarani dakika chache zilizopita, kidogo ilinikumbusha jambo fulani. Moja ya ibada zangu za kwanza za uponyaji nilizopata kuwa nazo, ilikuwa Georgetown, Indiana. Na ni wangapi wanaokumbuka mkutano wa Kisitu cha Wolfe nje hapa, nilipokuwa huko nje kwenye Kisitu cha Wolfe? Kuna mkono wa mtu fulani kule nyuma, wawili ama watatu wao; tulipokuwa huko kwenye Kisitu cha Wolfe. Ninaamini walikuwa na maskini mama mmoja, aliyeishi huku juu New Albany, alikuwa kiwete kwa miaka thelathini na mitano; akatembea kwa mara yake ya kwanza. Ama, alikuwa mbilikimo, naamini alikuwa hivyo, wala kamwe hajawahi kutembea.

3 Vema, bado nina Ujumbe ule ule usiku wa leo, "Yesu alikufa apate kuokoa na kuponya," wala sijaubadilisha hata kidogo. Tangu wakati huo, kumekuwa na mambo mengi ambayo yamefanyika. Nimeona zaidi ya watu milioni moja wakiletwa kwa Yesu Kristo, na ishara na maajabu kote ulimwenguni. Wafalme na watawala na viongozi wameombewa, na kuponywa kwa neema ya Mungu wetu. Nasi tuna furaha sana, usiku wa leo, kujua ya kwamba Mungu angali ni Mungu, wala Yeye habadiliki.

4 Nina furaha, usiku wa leo, kumwona rafiki yangu, Dk. Cauble, hapo. Sijui kama kuna mtu yeyote amemtambulisha au la, kutoka Kanisa la Mlango Uliofunguliwa, huko Louisville. Je, umetambulishwa, Ndugu Cauble? Naomba usimame kwa muda mfupi tu. Si—sitaki kumtahayarisha. Lakini, Dk. Cauble, kutoka Kanisa la Mlango Uliofunguliwa. Karibu kila mtu anamjua, nadhani, katika eneo hili, kwa sababu ana huduma ya redio, na huduma ya kipekee sana.

5 Na halafu nafikiri, tumekuwa na ibada nzuri sana huko Louisville, Kentucky, pamoja na Dk. Cauble. Daima ni furaha kuwa naye kwenye mikutano. Halafu, hawa wahudumu wengine hapa, pia, nadhani baadhi yao wanatoka katika makanisa ya huku. Na, enyi ndugu, huenda nisiwajue, lakini nina furaha kuwa mko hapa, na kutazamia wakati huu mdogo wa ushirika pamoja. Kidogo ni taarifa ya haraka. Sikujua hadi juzi, naamini ndivyo, kwamba nilikuwa nikishuka kuja huku.

6 Naye Ndugu yetu Arganbright, nanii wenu. . .mmoja wa wavulana wenu hapa kutoka mahali hapa, kutoka katika ujirani, mbona, unajua jinsi anavyofanya kazi, haraka sana.

Jinsi tu Roho anavyoonekana kumwongoza, mbona, yeye huanza kusonga mbele.

7 Hivi majuzi, nilikuwa. . .Loo, miezi sita ama minane iliyopita, nilikuwa nimeketi nyumbani, siku moja. Nami nilikuwa tu nikijiandaa kwenda Denver, Colorado, kwenye mkutano mkuu. Ndipo maskini jamaa huyu akaja nyumbani, akasema, "Ndugu Branham, nina ufunuo mkuu kutoka kwa Bwana."

Nikasema, "Naam, bwana."

8 Akasema, "Bwana anaweka Zurich, Uswisi, moyoni mwangu, niende huko." Kasema, "Unataka kwenda pamoja nami?"

9 Nikasema, "Vema, nina usiku mmoja huko Denver. Na kisha niende kwenye mkutano mwingine," nikasema, "sio muhimu sana. Kwa nini?" Kadiri nilivyowazia juu yake, mbona, ilionekana kwangu, kwamba kama nilijua kama Ndugu Arganbright alikuwa na ufunuo wa jambo fulani, ulikuwa ni mzuri, nao ulitoka kwa Mungu.

10 Nasi tukaenda Uswisi, naye Bwana akatupa waongofu elfu hamsini. Tukaenda, kutoka pale, mpaka Karlsruhe, Ujerumani, Naye akatupa yapata elfu hamsini zaidi, kitu kama hicho. Tukapata waongofu laki moja katika uamsho huo mdogo. Jinsi alivyotubariki! Na—na sasa tunapanga, msimu huu wa kiangazi, au mapema msimu huu wa kupukutika majani, kurudi Afrika, na Uswisi, India, ziara nyingi nchini kote.

11 Ninaenda sasa Minneapolis, Minnesota, huko juu kwenye uwanja fulani kwa ajili ya ibada ijayo. Kisha, kushuka, Maporomoko ya Sioux. Huko Meksiko ya kale, hadi kwenye Jiji la kale la Meksiko, uwanja wa michezo kule. Tunarudi, kwenda Pwani ya Mashariki. Na kisha, kutoka huko, hadi Anchorage, Alaska. Kisha tutakuwa na mikutano kadhaa ya Marekani. Tuna baadhi ya. . .hema mpya inayokuja, inayoenea watu elfu kadhaa, na baadhi ya magari, na kadhalika, kwa ajili ya mikutano michache ya Marekani kabla ya kurudi kwenye nchi za ng'ambo.

12 Kwa hakika tunaomba maombi yenu nyinyi watu wa huku. Hawa ni watu wa nyumbani, mnajua, kurejea nyumbani tena, na kwa hakika tunayathamini maombi yenu.

13 Na tunapoingia katika ibada hizi ndogo za baina ya makanisa ya kiinjilisti, hatuji kuwakilisha kanisa lolote, madhehebu yoyote, makundi yoyote maalum ya watu. Tunakuja tu kwa sababu tunampenda Yesu, nasi tunajua kwamba mnampenda Yeye, pia. Na tunakuja mahali hapa kwa wakati wa ushirika, kushirikiana kwenye Neno Lake, na kwenye baraka Zake zilizoahidiwa. Na mimi ni. . .Hilo ndilo lengo pekee tulilo nalo, ni kwa ajili ya mikutano hii.

14 Nasi tunafurahi usiku wa leo, kuwa na Ndugu Tommy Nickelson pamoja nasi, hapa, ambaye nina hakika ametambulishwa na Ndugu Arganbright, ambaye ni m—mhariri wa *Sauti* ya Wanaume Wakristo, kimataifa. Kundi la watu ambao ninajivunia kuwa mtu wao. Ni—ni Wafanyabiashara Wakristo ambao wameunda shirika lao, nalo limekuwa jambo la kimataifa. Wananifadhili katika mikutano yangu mingi kote ulimwenguni. Naye ndiye mhariri wa *Sauti* ya Wanaume Wakristo.

15 Na kwa hiyo tumekuwa nje, leo, tukipata shuhuda za magonjwa ya kale, kuona kama uponyaji wa Kiungu unadumu au haudumu. Tulishuka hadi kwa Bibi Carter. Natumaini wako hapa usiku wa leo, Georgie na Bibi Carter. Na Georgie ni mmojawapo wa wagonjwa walioponywa, naamini, yapata miaka kumi na minne, kumi na mitano iliyopita.

16 Na mmoja wa watu wenu wa mahali hapa, Bw. Hall, ambaye alikuwa mmoja wa waongofu wa kanisa la Kibaptisti la Milltown, ambako nilikuwa nikifanya uchungaji. Naye aliponywa hapa miaka michache iliyopita, kutokana na kansa; alikatiwa tamaa Louisville, na madaktari, na kote nchini. Naye ni mzima, hapa, usiku wa leo, mwenye afya na mkunjufu. Ninamwona ameketi hapa sasa.

17 Nasi tukaenda mpaka mahali ambapo Malaika wa Bwana alishuka na kuniambia la kufanya.

18 Na sasa, marafiki Wakristo, kuhusu jambo hili, tunalifikia jambo hili. Hatudai kwamba tunaweza kufanya uponyaji wowote, kwa kuwa huduma yetu ya wahudumu haiangazii uponyaji wa Kiungu, bali tunaamini katika uponyaji wa Kiungu kwa sababu ni Injili. Wala hakuna mtu anayeweza kumponya mtu yeyote. Uponyaji haupo katika uwezo wa mwanadamu. Uponyaji upo katika Nguvu za Mungu. Wala Mungu hampi mwanadamu uwezo wa kuponya.

19 Mungu alimpa Kristo pekee a—agizo la kuja duniani, kufa badala yetu, kwa ajili ya dhambi zetu na magonjwa yetu. Maandiko yalisema, “Alijeruhiwa kwa makosa yetu, kwa kupigwa Kwake sisi tuli-,” *tuli-* ni wakati uliopita, “tuliponywa.” Nasi tunaamini ya kwamba juu ya kukiri kwa imani, ya kwamba Yesu, Kuhani wetu Mkuu, amekufa na kufufuka tena, kuondoa dhambi ulimwenguni; naye ameketi mkono wa kuume wa Mungu, Baba, huko akituombea tunapokiri. Na alipokufa kwa ajili ya dhambi zetu, asingeweza kufa kwa ajili ya dhambi bila kufa kwa ajili ya ugonjwa.

20 Ugonjwa hutokana na dhambi. Sasa, labda hujatenda dhambi, ndiyo inayokufanya uwe mgonjwa. Lakini ilikuwa ni kwa sababu ya dhambi, kwanza kabisa, ndiyo iliyoleta ugonjwa duniani. Kabla ya kuwa na dhambi yoyote, hatukuwa na ugonjwa. Lakini ugonjwa ulipoingia, dhambi ni matokeo yake.

21 Na, sasa, huwezi kushughulika na dhambi, kwa njia yoyote, bila kushughulika na ugonjwa au kila tokeo ambalo dhambi ilisababisha. Dhambi, tunaposhughulika na dhambi, tunakabiliana na kifo. Tunaposhughulika. . .Nao ugonjwa ni ha—hatua ya kwanza ya mauti, wakati ugonjwa unapoushika mwili wako.

22 Katika usiku kama huu, kwa kusanyiko moja dogo, taarifa ya siku mbili kwenu ninyi watu kuja huku na kukusanyika jengoni, usiku wa leo. Itakuwa ni vigumu kujaribu kueleza kwa utondoti, ambalo tungefanya katika miamsho ambapo tunakaa kwa majuma na majuma, kuelezea, "Ugonjwa ni nini? Unatoka wapi?" Hakuna kitu kisicho na sababu yake, na kuna chanzo chake. Wala huwezi kupata tiba mpaka upate chanzo chake.

23 Nilikuwa nikisema, hapa si muda mrefu uliopita. Kama ningeenda kwa daktari. . .Hakika siwapingi madaktari. Madaktari wa upasuaji, upasuaji, hospitali, yote ni mipango ya Mungu. Lakini kama ningeenda kwa daktari na kumwambia kuwa nina maumivu makali ya kichwa ya mara kwa mara, naye anipe aspirini, na kusema, "Sasa, nenda zako, Billy, hii itakuwa sawa." Sasa, mtu huyo ananiondoa. Unaona? Yeye, ninii. . . Daktari halisi angeweza kuubaini ugonjwa wangu na kuona nilikuwa na shida gani. Na kisha angechunguza kabisa, mahali ulipo, halafu basi aanze kufanya kazi kutoka hapo.

24 Vema, sasa, hivyo ndivyo tunavyopaswa kufanya kazi ka—katika uponyaji wa Kiungu, au katika wokovu wa nafsi. Kama mtu akija na kusema kwamba amefadhaika sana juu ya wokovu wa—wake, jambo la kwanza kufanya, ninyi wahudumu mnalofanya, unashuka moja kwa moja mstarini mpaka unapata, hapa nyuma, mahali alipoenda kombo ama kile kilichotukia. Kuanzia hapo unalileta. Hivyo ndivyo ilivyo katika uponyaji wa Kiungu.

25 Ambapo, uponyaji wa Kiungu si nguvu fulani ambazo Mungu amempa mwanadamu. Uponyaji uko katika upatanisho peke yake.

26 Ninataka kuwaulizeni jambo fulani, maana ninajua kuna wahudumu hapa kutoka katika makanisa mbalimbali. Basi ungehubirije wokovu wa nafsi? Kitu pekee. . .Hungeweza kusema. . .Tunasema, "Vema, niliongoka, Ndugu Branham. Niliokoka miaka kumi iliyopita. Niliokoka miaka ishirini iliyopita." Hapana, hilo ni kosa. Uliukubali, labda, miaka kumi au ishirini iliyopita. Lakini, uliokolewa miaka elfu moja na mia tisa iliyopita, wakati Yesu alipokufa pale Kalvari. Alitatua suala la dhambi, milele, pale. Hapo ndipo alipolipa gharama kuu, akatoa ile dhabihu kuu, kusudi, kupitia kifo Chake pale Kalvari, basi tuna haki ya wokovu. Gharama imelipwa.

27 Kwa hivyo, si kile unachofanya. Ni yale aliyofanya Yeye. Na imani yako binafsi, na kukubali hilo, huleta wokovu wako. Na

sasa, kwamba, "Alijeruhiwa kwa makosa yetu; kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa." Mnaona?

28 Mara nyingi nimetoa tamshi hili, ya kwamba usingeninii—ya kwamba usingeweza kwa njia yoyote. . .Kama nyoka, au mnyama fulani alikuwa ameniparura kwa makucha yake ubavuni mwangu, naye alikuwa akiukata ubavu wangu na kuniua, hakuna haja ya mimi kujaribu kukata makucha yake. Mgonge tu kichwani. Kiue kichwa chake; inaua mwili mzima.

29 Vema, hivyo ndivyo ilivyo kwa uponyaji wa Kiungu. Yesu aliposhughulikia magonjwa au dhambi, pale Kalvari, ilimbidi kushughulika na kichwa chake, ambacho kilikuwa ni dhambi. Na, kwa kufanya hivyo, alishughulikia magonjwa pamoja nayo. Haikumbidi kuyakatilia mbali makucha. Aliua tu kichwa; hilo likashughulikia mengine. Kwa hiyo, Yesu alikuja, kuleta kwa jamii ya wanadamu, kila kitu ambacho—ambacho jamii ya Adamu ilikuwa. . .au, dhambi ya Adamu iliharibu katika bustani ya Edeni. Na sasa tunayo matokeo, ama arabuni ya wokovu wetu wa Milele, tunapomkubali Kristo kama Mwokozi wetu, au Kristo kama mponyaji wetu. Tuna hizo, pesa za arabuni ya ukombozi wetu wote, atakapokuja.

30 Tunajaribiwa. Sisi sote tunajaribiwa. Sisi sote tunatenda dhambi. Hakuna asiye na dhambi. Kila siku tunatenda dhambi. Paulo alisema ilimbidi "kufa kila siku." "Na tukisema kwamba twatenda dhambi, wala hatuna dhambi, basi" Biblia inasema, "tunamfanya Mungu kuwa mwongo." Wala tusingeweza kufanya hivyo. Kwa hiyo, tunatenda dhambi kila siku. Na ni neema, neema ya Mungu, inayotuokoa.

31 "Na tunapokiri makosa yetu, Mungu ana haki ya kuyasamehe." Na maungamo ya—yako, maadamu yangali mema, wokovu wako ni mkamilifu. Sawasawa na ilivyo kwa uponyaji wa Kiungu. Ni imani yako binafsi katika Bwana Yesu aliyefufuka.

32 Kwa hiyo, usiku wa leo, nilifikiri ningefanya tu. . .Katika kuwa na wakati huu mdogo wa ushirika pamoja nanyi, na mahali hapa ambapo makanisa yote yanaweza, kundi hili dogo la watu, linaweza tu kukusanyika pamoja hapa katika mji mdogo wa—wa Georgetown. Na, sisi, kwanza tunataka kushukuru Ndugu Arganbright na wale walioufanikisha huu. Tunataka kuwashukuru halmashauri ya shule kwa kuturuhusu kuchukua chumba hiki cha mazoezi ya viungo, usiku wa leo, kwa ajili ya ibada hii. Nami ninataka kumshukuru kila mhudumu aliye hapa, na kila mshiriki wa kanisa lolote, iwe ni Mprotestanti, Mkatoliki, kama ni Mwothodoksi, Myahudi, chochote kile. Tunawashukuru kwa kuwa hapa, na tunataka mjue kwamba hatutumii mbinu zozote wala masharti kwenye dini ya mtu yeyote. Chochote unachoamini, maadamu unamwamini Bwana

Yesu Kristo, Naye ni Mwokozi wako, wewe ni ndugu na dada yangu. Na, kwa hiyo, hivyo ndivyo tunavyoamini.

33 Na sasa tuna Neno Lake lililobarikiwa hapa mbele yetu. Sasa, kuna mtu yeyote anayeweza ku—kuvuta hiyo kwa kidole chake, angeweza kuifungua *hivi*, lakini hakuna mtu awezaye kukifungua hiki Kitabu, apate ufahamu, isipokuwa Kristo Mwenyewe. Biblia iliandikwa kwa uvuvio. Kwa hiyo, na tuinamishe tu vichwa vyetu kwa muda kidogo, kuzungumza na Mwandishi, kabla hatujakifungua Kitabu Chake.

34 Baba yetu wa Mbinguni mwenye fadhili, tumekusanyika hapa katika jina la Mwanao mpendwa, Bwana Yesu, Ambaye alikufa bure kwa ajili ya dhambi na makosa yetu. Alikufa ili atuokoe na maisha ya dhambi, naye angetupeleka Nyumbani Mbinguni, siku fulani tukufu katika Kuja Kwake. Alikufa, pia, ili kwa kupigwa Kwake tupate kuponywa magonjwa yetu. "Naye alijeruhiwa kwa makosa yetu. Alichubuliwa kwa maovu yetu. Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake. Na kwa kupigwa Kwake sisi tulipona," asema nabii.

35 Sasa, tunakuomba Wewe, Baba wa Mbinguni, uturehemu, na kwamba tuna usiku huu mmoja tu wa kukusanyika hapa katika jiji hili. Tunaomba kwamba utawabariki wale ambao wamefanikisha hili kwa ajili ya hili kusanyiko, na pia wale ambao wamekusanyika pamoja nasi, kushiriki katika Neno. Nasi tunaomba, Baba, ya kwamba utambariki kila mtu aliye katika Uwepo wa Kiungu, pia. Na jalia iwe ni usiku utakaokumbukwa kwa muda mrefu. Jalia uwe usiku kama wa kule kukusanyika kwa mitume wa siku zilizopita, wakati watu walipokusanyika pamoja, makundi madogo.

36 Usiku mmoja wakati Mtakatifu Paulo alipokuwa akihubiri hadi usiku sana, kijana, tunafundishwa, alianguka kutoka kwenye orofa ya juu, na uhai wake ukaondolewa kwake. Kisha Paulo akaweka mwili wake juu ya huyo mvulana, ndipo Mungu akamrudishia uhai wake.

37 Tunashukuru kuwa na Injili iyo hiyo, usiku wa leo, kuwahubiria watu, ya kwamba Mungu angali yu hai na anatawala. Anaponya wagonjwa. Anatusamehe dhambi zetu zote. Na, Baba, tunaomba, usiku wa leo, ya kwamba utatubariki kama watu.

38 Na, sasa, Wewe umesema katika Neno Lako nyenyekevu, hivi, "Mkimwomba Baba neno lolote katika Jina Langu, nitalifanya." Nasi tunaamini ya kwamba tuombayo, tunapokea, kwa maana ni kulingana na Neno Lake.

39 Na tunapoondoka hapa, usiku wa leo, katika makundi mbalimbali, katika kwenda kwenye makazi yetu mbalimbali, naomba ututembelee hivi kwamba tutakuwa na ushuhuda moyoni mwetu; na mazungumzo yetu, tunapoondoka hapa, yatakuwa kama wale waliotoka Emau katika ule ufufuo wa

kwanza, wakiisha kukutana kwa mara ya kwanza na Bwana Yesu aliyefufuka. Wao walisema, "Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, aliposema nasi njiani?" Naomba uzungumze na kila moyo usiku wa leo, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Mwanao mpendwa, Bwana Yesu. Amina.

40 Kufungua kwenye Injili ya Yuda Mtakatifu, katika Biblia, ambacho ni kitabu kimoja tu, mlango mmoja. Na katika kifungu cha 3 cha mlango huu, ningependa kusoma kwa ajili ya somo dogo tu, kupata muktadha kutoka kwake, kwa kile ningependa kuzungumzia kwa dakika chache zijazo. Kisha tutawaombea wagonjwa.

> *Wapendwa,. . .nilifanya bidii sana kuwaandikia habari ya wokovu ambao ni wetu sisi sote, naliona imenilazimu kuwaandikia, ili niwaonye kwamba mwishindanie kwa bidii ile imani. . .iliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu.*

41 Bwana na aongeze baraka Zake kwenye Neno Lake. Haya yaliandikwa miaka thelathini na mitatu baada ya Siku ya Pentekoste, baada ya kumwagwa kwa Roho Mtakatifu juu ya watakatifu wa mwanzoni. Yuda anajiita mtumishi, na ndugu, wa Yesu Kristo, naye aliandika Kitabu hiki kwa ajili ya Kanisa, na kuwaambia ya kwamba inawapasa kuishindania kwa bidii. Mahali pekee, katika Maandiko matakatifu, ambapo paliwahi kutwambia "shindanieni." Kwa sababu, hatupaswi kuwa na ugomvi kati yetu. "Bali kushindania kwa bidii kusudi fulani, Imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu." Na, kwamba, hatupaswi kushindana, wala hatujaribu kushindana, lakini tunataka kukabiliana na hili.

42 Kama ikinibidi kuuliza, usiku wa leo, "Ni Wamethodisti wangapi walikuwa kwenye umati huo? Ni Wabaptisti wangapi walikuwa kwenye umati huo? Wanazarayo wangapi? Wapilgirim Holiness? Katoliki?" mikono ingeinuliwa juu. Na hata kundi hili dogo la watu hapa, usiku wa leo, kungekuwako na mikono mingi itakayoinuliwa. Na kila mmoja wetu, katika madhehebu yetu mbali mbali, tungetaka kusema kanisa letu lilikuwa likiishindania ile Imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu. Ningetaka kulisema hilo kuhusu kanisa la Kibaptisti, na mtu mwingine angetaka kulisema kuhusu kanisa la Methodisti, mtu mwingine kuhusu kanisa Katoliki, na mwingine kuhusu. . . Ingekuwa hivyo katika makundi madogo ya watu. Sasa, ninataka kuamini ya kwamba sote tunaishindania Imani hiyo. Ninaamini kwamba kila mmoja anaishindania, vizuri sana kadri wajuavyo, kwa ile Imani.

43 Lakini, katika jambo hili, tukiona madhehebu mengi sana mbalimbali, hapana budi kuwe na kitu cha kweli na kitu cha uwongo. Sasa, hivyo ndivyo ninavyojaribu kuwa, ndugu yangu, dada, kwamba kuna. . .Hujawahi kuona mlevi asiye

mlevi wakati uo huo. Hujawahi kuona ndege mweusi mweupe. Hakuna kitu kama hicho. Wala hakuna kweli na uwongo uliochanganyika pamoja. Ama ni kweli au ni uwongo.

44 Na hivyo ndivyo ninavyomwamini Mungu. Kama sikuamini ya kwamba Yeye alikuwa ni Mungu yeye yule aliyeishi katika siku za Musa, ikiwa hakuwa Mungu yeye yule wa kutimiza kila ahadi aliyotoa, basi nisingeweza kuwa na imani ya kumkubali. Sasa, kuna ninii tu...Hiyo ni busara na hekima tu, kuwazia hilo...

45 Itatufaa nini usiku wa leo...? Huko hapa ili upate kuonekana tu. Hamngekuja kwenye mvua hii na kukusanyika mahali padogo kama hapa, mpate tu kuonekana. Mko hapa kwa kusudi moja, ambalo ni kupata kitu kizuri. Nami naomba kwamba Mungu atawapa kila mmoja wenu kitu kizuri sana ambacho hamtasahau kamwe. Na kila mmoja wenu Wakristo, na ainue furaha yenu Kwake, kukufanya umtumikie Yeye vizuri sana kuliko vile umewahi kumtumikia maishani mwako mwote.

46 Sasa, ingefaa nini kumtumikia Mungu aliyemtumikia Musa...Mungu ambaye Musa alimtumikia, na iwapo hakuwa ni Mungu yeye yule leo? Ingefaa nini kumtumikia Mungu wa kihistoria, kama Yeye si...kama Yeye hana nguvu, na ametoweka, na amekufa leo hii? Nataka kuwaulizeni swali hilo. Usingetaka kufanya hivyo, wala mimi. Ikiwa siwezi kumtumikia Mungu aliye hai na aliyepo hapa, ili kunisaidia ninapokuwa mhitaji, basi kuna faida gani ya kumtumikia Mungu?

47 Kama Yeye alikuwa ni Mungu, lakini Yeye si Mungu sasa; au kama alikuwa Mungu wa nguvu, amepoteza nguvu Zake sasa, kuna kitu kinachodhoofisha kuhusu Mungu huyo. Hiyo si ni kweli? Sasa tunataka kujadiliana. Kuna kasoro kama sivyo alivyo. Kama alikuwa, wala sivyo alivyo sasa, basi Mungu ana kasoro. Ikiwa...Ikiwa Mungu alikuwa shu—shujaa mkuu mwenye nguvu vitani, na alikuwa mponyaji mkuu wa magonjwa, Naye alikuwa mkuu katika sifa Zake zote, katika siku zilizopita, na kisha amepoteza nguvu Zake zote, wala Yeye si yeye yule leo?

48 Hata hivyo, Neno Lake linasema Yeye ni yeye yule leo, aliahidi kwamba angefanya mambo yale yale katika nyakati zote, mpaka atakapokuja tena. Ni jambo lisilopingika, katika Biblia. Waebrania, kumi na ta-...8:13, au 13:8, hasa, inasema kwamba, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo na hata milele." Hiyo ni kusema, yeye yule katika kanuni, yeye yule katika nguvu, yeye yule katika ufufuo, yeye yule katika uweza yote, yeye yule katika kuwepo kila mahali, yeye yule katika—katika—katika yote. Yeye ni—Yeye ni sawasawa na alivyokuwa. Na kila kitu alichokuwa wakati mmoja, ndicho alicho leo. Maandiko yanasema hiyo ni kweli. Mambo Yake yote ni yale yale. Sasa, kwa hiyo kama sisi...

49 Kila mmoja anataka kuamini hilo, lakini hata hivyo wanamwekea kikomo kwa kanuni za imani. Vema, wanasema, "Mimi ni mfuasi wa kanisa la Baptisti." Ninasema Baptisti, kwa sababu hilo ndilo kanisa nilimowekewa wakfu. Kasema, "Mimi . . . " Vema, Wabaptisti wanasema, "Vema, kanuni yetu ya imani ni sahihi." Wamethodisti wanataka kanuni zao za imani ziwe sahihi. Lakini tukimwekea Mungu mipaka . . . Kanuni hiyo ya imani, sina neno dhidi yake. Hiyo ni sawa. Lakini tukimwekea Mungu mipaka kwenye kanuni hiyo ya imani, basi tunamwekea Mungu mipaka, na tunajaribu kusema ya kwamba unaweza kutembea umbali *huu*.

50 Labda hatuna imani ya kutembea mahali ambapo Henoko alitembea, alipotembea kidogo pamoja na Mungu, alasiri moja, akaenda Nyumbani pamoja Naye, bila ya kufa. Na—na pia juu ya Yoshua, aliyezizunguka kuta za Yeriko mara kumi na tatu, na—na kupiga makelele sana hata hizo kuta zikaanguka chini. Huenda tusiwe na imani ya kuangusha kuta kwa makelele, huenda tusiwe na imani ya kutembea hadi Nyumbani pamoja na Mungu, lakini tusisimame njiani mwa mtu ambaye ana imani hiyo. E—endapo haikubaliani na kanuni yetu ya imani, nao wana imani, hima tuendelee moja kwa moja na tuamini, tuseme, "Bwana akubariki, ndugu yangu." Na kuendelea moja kwa moja, haidhuru yeye ni mfuasi wa kanisa gani. Hilo halileti tofauti yoyote, mradi tu yeye ni Mkristo na mwaminio. Na, je, wajua, rafiki Mkristo, hiyo ndiyo ulimwengu unayotaka kuona, leo hii!

51 Nilitua Bombay, India, ambako nilikuwa na umati mkubwa zaidi, wa watu laki tano. Umati mkubwa zaidi niliowahi kuhubiria, kwa wakati mmoja, maishani mwangu, ulikuwa huko Bombay. Nilipokwenda kule, huyu hapa akaja askofu wa kanisa la Methodisti, na mengi ya makanisa hayo makubwa. Akaja askofu mkuu, kanisa la Baniani, la Kibaniani pale, na wengine wengi wa makanisa makuu mashuhuri. Walikutana nami huko nje ambako maelfu ya watu walikuja kwenye uwanja wa ndege. Basi walipokuja, nao wakaniweka kwenye Hoteli ya Taj Mahal, ndipo wakakutana katika chumba kama hiki, pamoja na watu wote mashuhuri wa jiji hilo, na maraja na kadhalika.

52 Naye askofu wa kanisa la Methodisti, akasema, "Ndugu Branham, hatukupokei wewe kama mmishenari," akasema, "kwa sababu hatutaki kusikia neno 'mmishenari.'" Kasema, "Kwa sababu, ninyi watu wa Magharibi, pamoja na elimu yenu ya Kimagharibi, hamwelewi Maandiko kwa ufafanuzi wa kitabu cha mashariki." Na hiyo ni kweli.

53 Pamoja na theolojia yetu yote, kama ukiwahi kwenda Yerusalemu, ama kwenye nchi ya Mashariki, ambako Biblia hii iliandikiwa, ni Kitabu kipya kabisa kwako. Mawazo yetu ya Kimagharibi yako mbali na njia za Kimashariki. Hutaninii, huwezi kuelewa mifano, na kadhalika, mafundisho, mpaka uende huko na kuona desturi zizo hizo zikiishiwa siku hizi.

54 Na watu wengi wametuma. . .Sina chochote dhidi ya seminari, na wanafunzi, na nyumba za watawa, na kadhalika. Lakini, hayo yote, kamwe hawatamjua Mungu. Ni kujua tu katekismo, na kadhalika, namna hiyo.

55 Kumjua Mungu, ni kumjua huyo Mtu, Kristo, Mwenyewe. "Na kumjua Yeye ni Uzima." Si kujua kitabu chako cha kiada, ama kujua kanuni zako za imani, ama kujua katekismo yako; sio Uzima. Ni kumjua Kristo, yule Mtu, ni Uzima wa Milele. Na hilo ndilo tunalotaka kujua.

56 Sasa, askofu huyu aliniambia, akasema, "Kasisi Branham, juu ya theolojia," kasema, "tulikuwa na Biblia, miaka elfu moja mia saba kabla hamjawa taifa." Hiyo ni kweli.

57 Mtakatifu Tomaso alishuka. Nami nilisimama kanisani na kuhubiri ambamo Mtakatifu Tomaso, lile kanisa la asili, aliloanzisha huko India, aliposhuka kutoka Yerusalemu, kwenda India, na kuanzisha kanisa.

58 Naye akasema, "Tumekuwa na Biblia tangu wakati huo, pia tumekuwa na Ukristo tangu wakati huo, lakini," kasema, "uko katika hali duni huku India." Naye akasema, "Tumesikia kuhusu Dk. Reidhead, yule mtu aliyekuja kwako."

59 Ambaye alikuwa ra—rais wa Misheni kuu za Sudan, zilizo kuu zaidi ulimwenguni, ambaye alikuja kwangu. Naye akasema, "Ndugu Branham," kasema, "Nina digrii za kutosha hata ningeweza kukandika ukuta nazo; Daktari wa Theolojia, Dak-. . .Sha—Shahada ya kwanza, na kila aina za digrii." Kasema, "Nimesoma tangu nikiwa na umri wa miaka minane hivi. Lakini," akasema, "Ndugu Branham, Kristo yuko wapi katika hayo yote?" Akasema, "Kwani waalimu wamekuwa makosani?"

60 Nikasema, "Waalimu hawajakuwa makosani, bwana. Lakini, jambo ni kwamba, kamwe hutawahi kumjua Kristo kwa theolojia. Kamwe hutamjua Kristo kwa elimu. Inakupasa kumjua Kristo kwa tukio la kibinafsi, kuzaliwa mara ya pili kwa Roho Wake, anayeshuka na kuyabadilisha maisha yako na kukufanya kiumbe kipya katika Kristo Yesu. Hiyo ndiyo inayoleta tofauti." Hiyo ndiyo inayoleta tofauti kwenu.

61 Sasa, hiyo ndiyo sababu tuna madhehebu mengi sana pamoja na nadharia. Zote ni sawa.

62 Lakini, kitu halisi, Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, alisema (katika Yohana Mtakatifu, Injili ya Yohana Mtakatifu, mlango wa 4; ama mlango wa 3, kunradhi), alivyomwambia Nikodemo, "Mtu asipozaliwa mara ya pili, kwa maji na kwa Roho, hataingia kamwe katika Ufalme," haijalishi unahudhuria kanisa gani. Hayo ni Maneno ya Yesu Kristo Mwenyewe.

63 Sasa, *kuzaliwa*, kunamaanisha "kukombolewa kutoka kwa." Sasa, isipokuwa umekombolewa na Roho Mtakatifu, maishani

mwako, kuingia kwenye Maisha mapya katika Kristo, basi kanuni zetu za imani na kadhalika hazifai kitu. Lakini ni nzuri, ziko sawa, ni mafundisho ya maadili, na kadhalika, ambayo hutusaidia. Lakini, Kristo Yesu halisi, wa kibinafsi!

64 Na hiyo ndiyo imeifanya mikutano jinsi imekuwa siku hizi, na kusambaa kote ulimwenguni, ni kwa sababu, kwa neema ya Mungu, kutambulisha, kwa umati mkubwa au mdogo, Bwana Yesu aliyefufuka sasa hivi, wakati uliopo, katika nguvu Zake zile zile alizopata kuwa nazo. Hatuna haja ya kubahatisha.

65 Akasema, "Ndugu Branham, tunalo Neno. Tunayo Biblia," askofu alisema, huko India. "Lakini," kasema, "kinachotuvutia, sio theolojia yenu." Kasema, "Kinachotuvutia: je, Mungu amewatembelea ninyi Mayankii pamoja na Roho au karama ambayo inaweza kuifanya Biblia hii iishi tena?" Kasema, "Tunaijua Biblia." Kisha kasema . . .

66 Nikasema, "Vema, ndio kwanza ukubali kwamba hatuijui. Lakini, siijui vizuri sana, lakini namjua Mwandishi wake vizuri sana." Kisha nikasema, "Hilo ndilo jambo kuu."

67 Akasema, "Hilo ndilo tunalotaka kujua. Je, una imani ya kutosha, katika Mungu, kufanya ahadi hizi za Kiungu ambazo ametoa," kasema, "una imani ya kutosha kuzifanya halisi?"

Nikasema, "Kwa neema ya Mungu, Mungu atazitimiza."

68 Ndipo alasiri hiyo, nilikaribishwa na dini kumi na saba mbalimbali zilizokana Ukristo. Baadhi yao wanaabudu visubi, na wengine farasi, na wengine ng'ombe, na wengine Buddha, na Waislamu, na kadhalika. Na wote walikuwa na theolojia zao. Nzuri sana, kila kitu kilikuwa ni matendo, kitu fulani unachopaswa kufanya. "Fanya *hivi*. Fanya *vile*." Yote katika matendo; hamna neema kwake, hata kidogo.

69 Je, ninawapigia kelele sana? Kuna kurudishwa mwangwi tu. Na—natumaini siwapigii kelele.

70 Lakini, angalieni, usiku huo kwenye mstari wa maombi, wakati Bwana Yesu alipojitokeza jukwaani: Hao hapo maraja wameketi kwenye mito yao, na kadhalika. Na ilichukua zaidi ya saa mbili, kuwapanga mstarini, kufikia ambapo tungeweza kulifikia jukwaa la mnenaji. Basi wakati Bwana Yesu alipokuja na kumwambia mtu fulani, ambaye alikuwa kipofu kabisa kwa muda wa miaka ishirini; nikiona ono hilo juu yake, na kujua alikuwa anaenda kuponywa, nilimpa changamoto kila mmoja wao, aje akamponye mtu huyo. Bila shaka, walikaa kimya. Lakini Bwana wetu Yesu akayafumbua macho ya mtu huyo. Maelfu mara maelfu na maelfu wakamjia Kristo kwa wakati mmoja. Haya basi.

71 Sio suala la kama kanuni zetu za imani zinafanya kazi. Zitafanya kazi vizuri katika maisha ya maadili. Lakini kumleta

upya Bwana Yesu pamoja na ahadi Yake, ni kumjua Yeye, sio kanuni zako za imani.

72 Sasa, upesi kwenye somo letu, nami nitajaribu kuharakisha niwezavyo; na kuanzisha mstari, maana ni katikati ya juma, nanyi watu mnafanya kazi. Sasa, basi sikilizeni kwa makini. Fungu hilo la maneno linasema, usiku wa leo:

> *Wapendwa,*. . .*nilifanya bidii sana kuwaandikia habari ya wokovu ambao ni wetu sisi sote,*. . .

73 Huyu ni Yuda Mtakatifu, sasa, akiliandikia Kanisa, miaka thelathini na mitatu baada ya Pentekoste.

> . . .*na* kuwasihi *kwamba mwishindanie kwa bidii ile imani* (siyo imani *fulani*; *ile* imani) *waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu.*

74 Sasa, kila mmoja wetu, katika makanisa yetu, hayo ni sawa. Na—nami nataka uwe pamoja na kanisa lako na kuliunga mkono kanisa lako, na kulisaidia kwa utukufu wa Mungu.

75 Lakini sasa hebu turudi nyuma tupate kujua. Sasa, hapana budi kuwe na kitu, kama sisi. . .Alisema, "Mwishindanie kwa bidii Imani aliyokabidhiwa mtakatifu mara moja tu," basi hakika kuna njia fulani ya kujua hiyo "Imani" ilikuwa ni ipi. Sasa hebu turudi katika Biblia. Nafikiri hiyo ingekuwa ya kimantiki, na thibitisho la kutosha kwetu sote, tukirudi nyuma na kuona kile wale watakatifu. . .aina—aina ya Imani waliyokuwa nayo. Na kama "alitusihi kuishindania kwa bidii Imani hii," tukiona ni Imani ya aina gani waliyokuwa nayo, basi tunapaswa kuishindania Imani hiyo. Kwa maneno mengine, tuseme, "*Hii* ni kweli." Sasa tutaona ilikuwa ni nini.

76 Kabla hawajaitwa watakatifu, katika Biblia, walikuwa. . . Katika Agano Jipya, Yohana Mbatizaji alikuja kati ya torati na Kristo, ambalo lilikuwa ni pengo, au jiwe kuu la msingi lililofunganisha hivyo vipindi viwili vya wakati pamoja.

77 Sasa, inatubidi kuanza na Kristo, kama tutazungumza kuhusu Imani ya Kikristo, kwa sababu Yeye ndiye mwa—mwanzo wa Imani ya Kikristo.

78 Yohana alikuja, Yohana Mbatizaji, akahubiri katika nyika ya Uyahudi, wala hakufanya mwujiza hata mmoja, hakufanya ishara yoyote. Lakini aliyalaani tu makanisa, na kuwahukumu makuhani na marabi, na kadhalika. Na kuwaambia kuna Mtu ajaye.

79 Na kwenye ile ibada ya ubatizo, alipokuwa akibatiza, alimwona Yesu akija na Nuru ikimfuata. Naye akasema, "Tazama Mwana-kondoo wa Mungu, aondoaye dhambi ya ulimwengu."

80 Ndipo Yesu akabatizwa. Roho Mtakatifu akashuka kutoka Mbinguni. Na Sauti kutoka Kwake, ikisema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa, ambaye ninapendezwa kukaa ndani

Yake.” Tafsiri asilia inasema, “Ambaye ninapendezwa kukaa ndani Yake.”

81 Ambapo, “Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake.” Alikuwa Mungu katika mwili.

82 Sasa, sasa hebu tuone aliishi maisha ya namna gani. Nami nataka kuwaulizeni jambo fulani, ninyi watu, tunapozungumza. Jinsi Yeye alivyokuwa wakati huo, anapaswa kuwa vivyo hivyo. Kama hiyo ndiyo Imani aliyoitambulisha kwa ulimwengu, hiyo inapaswa kuwa ndiyo Imani tunayopaswa kushindania usiku wa leo. Hiyo ni kweli? Hiyo ni kweli. Inapaswa kuwa. Vema.

83 Sasa, tunaona, mara tu Yeye alipoanza katika huduma Yake. Tutaangalia alikuwa na huduma ya aina gani. Tutaanzia kwenye mlango wa kwanza wa Luka Mtakatifu, tukiinukuu kwa kumbukumbu. Unaweza kuisoma unapotaka. Luka Mtakatifu, mlango wa kwanza, inafundisha ya kwamba Yesu alianza kwenda huku na huko, akiwatendea watu mema. Angewaombea wagonjwa, nao wangepona. Sasa, hilo ni mojawapo ya mambo aliyofanya, kuwaombea wagonjwa. Basi siku moja . . .

84 Sasa, sikilizeni kwa makini sasa, maana itaninii . . . msiposikiliza kwa makini, kushika kila neno, itakuwa ni kikwazo kwenu, katika dakika ishirini au thelathini zijazo, mstari wa maombi utakapoanza. Mnaona? Sasa sikilizeni kwa makini.

85 Jambo la kwanza tunalomwona Yesu akifanya, baada ya kuwachagua mitume Wake wawili au watatu . . .

86 Na jina la mmoja wao lilikuwa—lilikuwa Filipo. Naye Filipo alikuwa mtu mwema, Mtakatifu Filipo. Naye alipoona na kujua ya kwamba huyo alikuwa ni Masihi, kwa maana alimwona akiwaombea watu nao wakipona, alizunguka, kama maili thelathini, kuzunguka nyuma ya milima ya Uyahudi, ndipo akampata rafiki yake aliyeitwa Nathanaeli. Naye Nathanaeli alikuwa chini ya mti, akiomba. Naye akasema, “Njoo umwone yule niliyempata: Yesu wa Nazareti, mwana wa Yusufu.”

87 Naye akasema, “Jambo lolote jema linaweza kutoka Nazareti?” Nathanaeli akasema.

Akasema, “Njoo, uone.”

88 Sasa, nadhani hilo ndilo jibu bora zaidi ambalo mtu yeyote angeweza kutoa wakati wowote; ni, kabla ya kukosoa chochote, njoo ukione, kwanza. Kiangalie, wewe mwenyewe. Ishi katika nuru ya Biblia, uone kama ni kweli.

89 Haijalishi inaonekanaje, au yale wanayosema wengine, dini ya Yesu Kristo haijawahi kuwa maarufu. Na haitawahi kuwa maarufu, kwa sababu ulimwengu unawajua walio wake. Mnaona? Nawe si wa ulimwengu, unapokuwa Mkristo. Wewe ni mtu tofauti, kutoka kwa ulimwengu. Tunajua hilo. Yesu alisema,

"Ninaomba, Baba, wasiwe wa ulimwengu." Kwa hivyo, ninyi si wa ulimwengu. Ulimwengu . . .

90 Biblia ilisema, "Ukiipenda dunia, au mambo ya dunia, kumpenda Mungu hata hakumo ndani yako." Hayo ni, Maandiko yanasema hivyo.

91 Kwa hiyo, "Huwezi kupenda mabwana wawili," Yesu alisema. "Huwezi kumpenda Mungu na mali." Neno *mamoni*, likitafsiriwa, linamaanisha "ulimwengu." Naye akasema, "Ama utamtumikia mmoja, na kumchukia mwingine," au vinginevyo. Yesu alisema hayo katika Mathayo Mtakatifu, mlango wa 5. Huwezi kumtumikia Mungu na ulimwengu kwa wakati mmoja. Lazima uwe mmoja au mwingine.

92 Basi Mungu aturehemu! Hiyo ndiyo shida ya watu wetu siku hizi, wanaoitwa Wakristo katika taifa hi—hili. Wanajaribu kuishi kama ulimwengu, na kudai kuwa Wakristo. Na hiyo ndiyo sababu asiyeamini, aliye nje, ana wakati mgumu sana kufanya uamuzi wake, ni kwa sababu anawaona watu wanaojiita Wakristo, hawaishi tofauti na walimwengu wengine. Hilo ni kali sana, lakini hilo ni kweli. Tunapaswa kukabiliana na kweli.

93 Labda kuna wanaume na wanawake wanaoketi hapa, sitawaona tena mpaka niwaone kwenye Hukumu. Na mimi—mimi sina budi kuwa mkweli na mwaminifu, kwa sababu sina budi kuikabili Hukumu na kukutana na maneno yangu tena kwenye Hukumu, kwa hiyo sina budi kuwa mkweli kuihusu.

94 Sasa, tunaona kwamba—kwamba Filipo, mara alipomwona Nathanaeli, alisema, "Njoo, umwone Yule niliyempata."

95 Ndipo Nathanaeli, akiwa mtu mwadilifu, mtu mwema, alisema, "Laweza neno lolote jema kutoka Nazareti?" Nazareti ulikuwa mji mbaya, mwovu, mbaya sana; wahalifu, majambazi, na kadhalika, waliinuka. Na—nao ulikuwa na makundi ya wahalifu, siku zile, waliotoka Nazareti, mji mbaya sana. Akasema, "Laweza neno lolote jema kutoka Nazareti?"

Akasema, "Njoo uone."

96 Sasa tunaweza kuuliza leo, "Laweza neno lolote jema kutoka kwenye kanisa la Methodisti? Laweza neno lolote jema kutoka kwenye kanisa la Baptisti, Presbiteri, ama kanisa lolote lile?" Jambo la kwanza kufanya ni kuja uone. Tafuta kujua.

97 Sasa lichunguze, si kwa taratibu zako za ibada, si kwa katekismo, si kwa moja . . . Lichunguze kwa Neno la Mungu.

98 Kwa maana, Biblia ilisema, ya kwamba, "Yeye atakayeondoa, ama kuongeza, chochote kilicho katika Kitabu hiki, Mungu ataliondoa jina lake katika Kitabu cha Uzima." Ufunuo, mlango wa 21, inasema ya kwamba atafanya hivyo; au, mlango wa 22, hasa, wa kitabu cha mwisho cha Biblia. Alisema, "Kama mtu yeyote . . . " Mungu Mwenyewe, akizungumza na huyo mwandishi, alisema, "Mtu akiongeza neno moja katika

Kitabu hiki, au akiondoa neno moja kutoka Kwake, Mungu ataliondoa jina lake kutoka katika Kitabu cha Uzima. Naye ataangamizwa." Kwa hiyo hatuna budi kudumu hasa na yale Maandiko yasemayo.

99 Sasa, alipompata Nathanaeli, na a—akasema, "Njoo, uone," hivyo akamfuata.

100 Sasa hebu tuangalie Yesu alikuwa mtu wa aina gani. Sasa, kama tulitaka kumwona Yesu usiku wa leo, kama tungeenda . . . Kama mtu fulani alitwambia Yesu Kristo alikuwa Georgetown, Indiana, ni nini . . . Naye alikuwa katika mwili wa mwanadamu kama sisi tulivyo, usiku wa leo, tungetaka kumwona mtu wa aina gani? Sasa, hili linaweza kuwa la kushangaza.

101 Lakini, tunakuja kutafuta mwanamume ambaye angekuwa amevaa tofauti kidogo na watu wengine wowote? Tusingekuwa tunamtafuta Yesu, au hatungempata, maana Yeye alivaa kama tu watu wengine. Hakukuwa na tofauti katika mavazi Yake.

102 Je, tungekuja kuwaona watu ambao walikuwa—ambao walikuwa wasemaji hodari? Wasemaji mashuhuri hodari? Hapana. Biblia ilisema, "Sauti Yake hata haitasikika barabarani."

103 Je, tungekuja kumwona mtu ambaye alikuwa a—akijisifia kanisa lake kuu na *kadhalika*? Hapana, bwana. Biblia ilinena tofauti sana juu Yake. Kasema, "Alikuwa ni Mtu wa huzuni, na—na ajuaye sikitiko." Hakuwa mtu wa makelele mengi, au harakati. Alikuwa Mtu mnyenyekevu. Naye alikuwa. Naye aliacha . . .

104 Je, tungempata miongoni mwa matajiri? Hakuwahi kuishi na matajiri. Walimpata wapi? Ungempata miongoni mwa maskini. Alishuka kando ya mto akawaona wavuvi.

105 Wazia juu ya kanisa kuu la Othodoksi, pamoja na makuhani wao wote mashuhuri na makuhani wakuu, na madoido yao makuu na utukufu, katika siku hizo. Wala hakuna wakati mmoja ambapo mtume yeyote ama mtu yeyote wa Mungu aliwahi kulitembelea, ama kulikubali. Mungu alipomtuma Mwanawe, alimtuma mbali nalo. Naye akawaambia kwa ukali ya kwamba walikuwa katika unafiki, na kuwaambia jinsi walivyokuwa wabaya, na kila kitu. Nao wakasema, kwamba, "Ana pepo, kwa sababu hata haamini katika kanisa letu." Mnaona? Nao walikuwa kanisa la siku hizo. Kwa hiyo, mnaona, huwezi kwenda na kanisa. Huna budi kwenda na Mungu. Hapo ndipo ulipo . . . na kwa Kristo.

106 Sasa, Nathanaeli alipokuja njiani, sasa tutaona alichokipata. Alimwona Mtu amesimama pale, akifanya jambo kinyume na yale kanisa lilikuwa likifundisha. Kanisa lilifundisha kwamba siku za miujiza zilikuwa zimepita. Lakini huyu hapa Yesu amesimama pale, akitenda . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

107 Inua mkono wako, popote pale jengoni. Sijali uko wapi. Inua tu mkono wako, useme, “Mungu, kwa hili, nataka uniponye, Mungu.” Hiyo ni kweli. Ni karibu tu kwa jumla, kila mahali. Nitawaambia mtakalofanya.

108 Niliwaambia kwamba Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, yuko hapa katika umbo la Roho wa Mungu. Je, hiyo ni kweli? Wakristo wangapi wanaamini hivyo? Hebu tuone mkono wako. Hilo ni sawa. Basi, kama Yeye yuko hapa, Naye ni Bwana Yesu yeye yule, basi ana . . . Yeye anawajibika kufanya jambo lile lile. Je, hiyo ni kweli?

109 Sasa, Yeye alisema asingeweza kuponya. Baba alimwonyesha, Naye akafanya yale ambayo Baba alisema. Je, hiyo ni kweli?

110 Sasa, anayesimama mstarini, namjua huyu mama wa kwanza anayesimama hapa. Wala sijui sasa kama namjua mtu mwingine yeyote au la. Nimemwona mama huyo, kama wa pili au wa tatu kutoka nyuma kule. Nilimwona. Sijui jina lake ni nani, lakini nimemwona. Nadhani hao ni kama tu wote ambao—ambao—ambao ninawajua. Na, hao ni kama tu wote ambao—ambao ninawajua. Vema.

Sasa hebu na tuinamishe tu vichwa vyetu kwa muda kidogo wa maombi.

111 Sasa, Baba wa Mbinguni, huu ndio ule wakati. Nimezungumza, kadiri nijuavyo mimi, juu Yako. Sasa, mpendwa Bwana Yesu, ninaomba ya kwamba utanisaidia, Wewe unajua ya kwamba sijui lolote kuwahusu watu hawa. Wakati mwingine najua ninii yao . . . wao ni akina nani. Sijui shida zao. Wewe wajua. Unaweza kusema chochote utakacho, nami najinyenyekeza na kujisalimisha Kwako, ya kwamba Roho Mtakatifu mkuu atakuja usiku wa leo na kumchukua maskini mtu huyu, asiyestahili, kwa ajili ya utukufu wa Mungu, na kutia upako. Wala usiniache ninene, midomo yangu mwenyewe, bali mwache Roho Mtakatifu anene na kuzifanya kazi ambazo Yesu Kristo Mwana wa Mungu alisema kwamba angezifanya kupitia kwa watu Wake, katika kila wakati. Ninaomba baraka hii katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

112 Sasa, nitawaulizeni jambo moja. Kama utasimama kwa uchaji, na kuwa mnyenyekevu, wala usiwe na shaka, na kuamini kwa moyo wako wote, basi Bwana Mungu wa Mbinguni bila shaka atauponya mwili wako na kukupa afya.

Sasa, ni imani yako. Sio . . . Unaona? Sasa jambo ndilo hili.

113 Sasa huyu hapa mama amesimama, na—naamini ninajua huyo mwanamke ni nani. Sina hakika, lakini ninaamini kwamba najua yeye ni nani. Na mimi—mimi—mimi . . .

114 Hiyo ni kweli, hivi sikujui, mama? Uh-huh. Vema, bwana. Ninaamini ninajua wewe ni nani. Jambo ndilo hilo. Vema.

Sasa, kama ungekuja hapa kwa dakika moja tu. Sasa, basi kujua jina lako, pasipo kukujua. . .Je, jina lako ni Seduf, au kitu kama hicho? [Dada huyo anasema, "Hapana, ni jina la dada yangu."—Mh.] Lo, naam, huyo ni dada yako. ["Ulinijua nilipokuwa Wilson."] Ulikuwa, na—naamini, si nilikujua nilipokuwa nikifanya kazi katika Kampuni ya Utumishi wa Umma, au chochote kile? ["Ndiyo."] Hiyo ni kweli. Nimeuona uso wako mahali fulani. Ni—niliujua. Nilidhani jina lako lilikuwa ni Seduf, lakini, Seduf ni dada yako. Je, hiyo ni kweli? ["Ndiyo."] Na jina lako lilikuwa Wilson.

115 Vema, nina furaha kukuona tena, dada. Sasa Bwana akubariki.

116 Sasa, mimi, kama ndugu yako katika Kristo, unajua ya kwamba sijui kilichokuleta hapa, sivyo? [Dada huyo anasema, "Hapana."—Mh.] Si—si—sijui. Hapana, mama. Ni—ni siri kwangu, ambayo siijui. Sasa, kama Bwana Yesu atanijalia kujua kilichokuleta hapa, na kile unachohitaji Kwake, kama Yeye atajidhihirisha sana hata—hata atatangaza unachohitaji, basi utakubali kuwa kinatoka Kwake? ["Ndiyo."] Utakubali. Vema.

117 Sasa kusanyiko linaisikia sauti yake, nanyi mnaona vinasa sauti vikiendelea. Hiyo ndiyo njia. Sasa tazama. Sasa, kama Yeye akinena lolote kumwambia mwanamke huyu, kilichomleta hapa, si ingekuwa ni Roho yeye yule aliyenena na yule mwanamke kisimani, aliyejua ilipokuwa shida yake? Hiyo ingekuwa sawa? Mnaona? Sasa, hiyo, basi, imani yake katika kile kinachofanyika, itaamua uponyaji wake.

118 Sasa kwenu mlio kwenye kusanyiko, ambao hamna kadi za maombi, mnaoamini kwa moyo wenu wote ya kwamba Yesu Kristo yuko hapa kukuponya, kama utaamini kwa moyo wako wote, haitakulazimu kuwa katika mstari huu wa maombi. Hakika haitakulazimu. Kitu pekee utakachopaswa kufanya ni kumwamini Mungu.

119 Sasa ningewaomba, kwa kuwa kuna kifafa hapa. . .Na mtu yeyote ambaye amekuwa mikutanoni, anajua kifafa kinavyofanya. Wakati mwingine huinuka. Kwa hiyo, sasa, iweni na kicho tu, kaeni kimya. Haidhuru kile kinachotukia, wewe kaa kimya. Unaona? Na umwamini tu Bwana Yesu na kuomba. Mwombe Baba wa Mbinguni akufadhili. Lakini, sasa, kama wewe ni asiyeamini, nisingekaa, unaona. Kwa hiyo, sasa, hii si kuigiza kanisa. Huu ni ukweli. Tunakumbana na vitu. Laiti ningalikuwa tu na dakika zingine chache, ama usiku mwingine, ambapo ningeweza kuwaeleza kuwa vitu hivi ni nini, hata muweze kuona jinsi vilivyo kwa matamshi ya Kimaandiko, (vimepewa majina ya kimatibabu), lakini jinsi vilivyo hasa mbele za Biblia.

120 Sasa, dada hapa amesimama mbele yangu. Sasa, sio telepathia. Hapana, bwana. Ninahisi hilo, nahisi hilo. Wewe, sasa, u—usingeweza kuyaficha maisha yako sasa hata ufanyeje. Unaona, Roho Wake yuko hapa sasa.

121 Ni wangapi wamewahi kuiona picha Yake, mahali walipoipiga? Nayo iko Washington, DC, Kiumbe pekee cha kimbinguni kilichowahi kupigwa picha, kinaweza kuthibitishwa, ulimwenguni. Wana hadithi za kubuni za watu kwenye kichaka, na yote kama hayo, lakini sikuzote imethibitishwa kuwa si kweli. Mnaona? Lakini waliipiga Hii, na wengi wenu hapa mlikuwepo wakati ilipopigwa.

122 Majuma machache yaliyopita, kamera ya Ujerumani iliipiga, huko Ujerumani, mara tatu mbalimbali. Na ni ile ambayo mnaiona katika picha, iko papa hapa sasa jukwaani. Kweli kabisa.

123 Sasa iweni na kicho. Msisogeesogee. Wawekeni watoto wenu karibu nanyi. Na mwe katika maombi, muone kile Roho Mtakatifu atatufanyia, usiku wa leo. Na kama . . .

124 Nami ninaomba kwamba Mungu atawabariki; na wakati mwingine, duniani, tutakutana tena. Niombeeni, tunapoenda hudumani baada ya ibada hii, huko nje hudumani, katika mikutano mikubwa, kuwaombea wagonjwa.

125 Na muwe na kicho, kila mtu, tafadhali, kwa maana tuko Mbele za Mwenyezi Mungu, Roho Mtakatifu ambaye sasa yuko karibu.

126 Bibi, jina lako lilikuwa nani sasa, Wilson? [Dada huyo anasema, "Cobb, sasa."—Mh.] Bibi Cobb. Bibi Cobb, e—endapo Roho Mtakatifu yupo sasa, atanijulisha jambo fulani la maisha yako, ambalo linaweza kukupa moyo wa kukufikisha mahali pa kukuruhusu kumwamini Bwana Yesu kwa ajili ya uponyaji wako. Au, sijui uko hapa kwa sababu gani. Inaweza kuwa ni shida za kifedha. Inaweza kuwa ni za nyumbani. Sijui. Lakini, Yeye anajua, sivyo? ["Naam, anajua."]

127 Ninaona jambo moja ambalo uko hapa kwa ajili yake, ni kwa sababu unasumbuliwa na ugonjwa wa fadhaa. Una wasiwasi sana, umefadhaika. Jambo jingine, una—una kikohozi cha pumu kinachokusumbua. Hiyo si ni kweli? [Dada huyo anasema, "Ndiyo."—Mh.] Hiyo ni kweli. Vema.

128 Sasa, unaamini kwamba kila kitu kiko sawa kwako sasa? Umeponywa sasa. Unaweza kwenda nyumbani. Yesu Kristo, imani yako, imekuponya. Nenda zako na uwe katika maombi.

129 Baba wa Mbinguni mwenye fadhili, katika Jina la Bwana Yesu Kristo, tunambariki huyu, dada yetu mpendwa, na kukuomba uwe mwema kwake, katika Jina la Yesu. Amina.

130 Njoo, bwana. U hali gani, bwana? Je, unaamini Bwana Yesu Kristo kuwa Mwana wa Mungu aliye hai? [Ndugu

huyo anasema, "Naam, bwana, ninaamini."—Mh.] Unaamini ya kwamba Yeye yuko hapa kukuponya? ["Ndiyo, ninaamini."] Uh-huh. Unaamini? ["Ninajua hivyo."] Unajua ya kwamba Yeye yuko hapa kukuponya.

131 Je, huyo ndiye mama aliyeombewa hivi punde? Ulikuwa yule mama pale? Uh-huh.

132 Una shida ubavuni mwako, unayeketi hapo karibu naye, sivyo, bwana? Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kukupa afya na kukuponya? Alipopitia karibu nawe wakati huo, ulikuwa na hisia ya ajabu, sivyo? Huyo alikuwa ni Roho Mtakatifu. Ulikuwa na shida ubavuni mwako. Sasa, imekuacha sasa, bwana. Imani yako imekuponya. Hiyo ni kweli? Inua mkono wako. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Vema, bwana.

133 Simjui mtu huyo. Sijawahi kumwona maishani mwangu, lakini Yesu Kristo amemponya. Vile vile tu imani yake ilivyomgusa Bwana Yesu, katika siku zilizopita, yule mwanamke mwenye kutokwa na damu, vivyo hivyo imani ya mtu huyo iligusa wakati uo huo. Haikubidi kuninii . . .

134 Unawazia nini, maskini mama uliyesimama hapo kwenye mstari wa maombi, ukiwa na koti juu ya bega lako? [Dada huyo anasema, "Ukweli mtupu."—Mh.] Uh-huh. Ndiyo. ["Ulichosema ni Ukweli. Ninaamini kila neno Lake."] Mungu akubariki.

135 Huyo mama aliye nyuma yako hapo, ameinua mkono wake juu, namna *hii*. Uh-huh. Ungependa kuondokea operesheni, sivyo? Unafikiri uvimbe huo, Mungu angeweza kuuondoa kwako, bila upasuaji? Unaamini Mungu angekuponya? Una uvimbe, sivyo? Na, naam, hiyo ni kweli. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya bila upasuaji? Unaamini? Je, utamkubali Yesu sasa hivi, kama mponyaji wako? Utamkubali?

136 Baba wa Mbinguni mwenye fadhili, imani ya mwanamke huyo iligusa hapa, nami nikaona ono mbele yake, naye daktari akipafingirisha mahali pale kwa ajili ya upasuaji wake. Ninaomba, Baba wa Mbinguni, kwamba, katika Jina la Yesu Kristo, ya kwamba utamponya huyu mwanamke bila upasuaji, kwa ajili ya Utukufu Wako. Amina.

137 Unaweza kuketi sasa. Haikubidi kuja kwenye mstari wa maombi. Imani yako inakuponya. Amina. Mungu akubariki.

138 Unamwamini Bwana Yesu? "Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana."

139 Mama, unayesimama; ulivunja mkono wako. Una mkono ulioumia hapo, sivyo, mama? Uh-huh. Umetoka Corydon, sivyo? Una mtu fulani pamoja nawe, aliyeambatana nawe, sivyo?

140 Anaugua ugonjwa wa fadhaa. Hiyo si ni kweli? Ikiwa ni kweli, inua mkono wako. Vema. Sasa unaweza kutoka na kurudi nyumbani, uponywe, pia, mama. Amina.

141 Ni imani yako, ndivyo. Hiyo, sasa, hiyo ndiyo ninayozungumzia, Roho Mtakatifu.

142 Bwana? Unaweza kuamini tatizo lako la moyo limekuacha, nawe utakuwa mzima? Unaamini? [Ndugu huyo anasema, "Naam. Naamini."—Mh.] Vema, bwana, basi unaweza kuondoka. Amina.

143 Hebu tuseme, "Mungu asifiwe." [Kusanyiko linasema, "Mungu asifiwe."—Mh.] Sote tuombe.

144 Mama unayekuja, u hali gani? Nadhani hatufahamiani. Sivyo, mama? Sijawahi kukuona maishani mwangu. Hunijui kabisa. Kama tu . . . Bwana wetu Yule aliyesimama kisimani na kuzungumza na mwanamke yule. Na kusema, alisema . . . Alisema, "Nipe maji ninywe." Alitaka kuongea naye. Sasa, hii ikiwa ndiyo mara yetu ya kwanza kukutana maishani, ni mwanamume na mwanamke tena, hiyo si ni kweli? Vema, basi, ikiwa Yesu Kristo amefufuka katika wafu, naye aliahidi kwamba atakuwa pamoja nasi, ndani yetu, mpaka mwisho wa dunia, nasi tungefanya mambo yale yale aliyofanya, ingebidi iwe ni kitu cha aina ile ile.

145 Basi, kama Yesu alisimama hapa Naye alikuwa amevaa suti hii aliyonipa, jambo pekee angaliweza kufanya, kuhusu . . . kama wewe ni mgonjwa na unahitaji uponyaji, angekwambia, "Nilifanya hivyo pale Kalvari, mtoto. Je, ungeamini?" Sasa, lakini, sasa, Yeye angeweza kukwambia jambo fulani, labda tatizo lako, ama chochote kile, sababu ya wewe kutoponywa. Lakini, mimi, nikiwa mgeni kwako, ingekuwa vile vile tu. Hiyo si ni kweli?

146 Sasa, kila mtu awe na kicho sana sasa. Kumbukeni, mko Mbele za Bwana. Na Injili ile ile niliyowasomea, usiku wa leo, mnaiona ikiishi upya. Mnaona?

147 Sijawahi kumwona mwanamke huyo. Sijui lolote kumhusu, sijawahi kumwona maishani mwangu. Mungu anamjua; simjui. Lakini, sasa ningezungumza naye, ili kuwasiliana na nafsi yake.

148 Upako ulio hapa pamoja nami sasa ni yule Malaika wa Bwana, ile Nguzo ya Moto iliwafuata wana wa Israeli, ambayo ilikuwa ni Kristo katika umbo la Roho; akashuka, akafanyika mwili; akarudi kwa Baba; akarudi tena kuishi katika Kanisa Lake, jambo lile lile. Sio mimi; ni Yeye.

149 Simjui mwanamke huyo, sijui lolote juu yake; nina elimu ya darasa la saba. Angalia hawa watu, unasema . . .

150 Vema, huko nje kwenye kusanyiko, wana—wanaponywa. Wakiwa tu wameketi kwenye kusanyiko, wakisimama popote wawezapo. Mungu yuko hapa kuponya, hivyo tu, kama unaweza kuamini.

151 Ninamwona mtoto anayeteseka, lakini siwezi kusema kuwa amepona; sijui bado. Ikiwa utaendelea kuomba, mama, ukiamini kwa moyo wako wote.

152 Sasa, kwako tena, dada, kuzungumza nawe. Sasa, kumekuwa na njaa moyoni mwako, kwa muda mrefu. Njaa hiyo ni maisha ya karibu zaidi pamoja na Mungu. Umejaribu kiasi hicho; ukajaribu na kushindwa; ukajaribu na kushindwa. Hiyo si ni kweli? [Dada huyo anasema, "Ndiyo."—Mh.] Uh-huh. Masumbuko maishani.

153 Hapa wakati fulani uliopita, ulikuwa ukiomba mahali fulani, kwa sababu ulikuwa unakabiliwa na jambo zito, kama vile upasuaji au kitu fulani. Naam, ndiyo, nauona, daktari, amechunguza, una kitu fulani kwenye, ni mguu wako, kiko kwenye mguu wako wa kulia, ndilo tatizo ambalo unaenda kufanyiwa upasuaji. Ulitoa ahadi, kama Mungu angekujalia kupona, ya kwamba utamtumikia na kuishi maisha ya karibu zaidi. Sisomi mawazo yako. Hiyo ni kweli, sivyo? [Dada huyo anasema, "Ninaamini."—Mh.] Hiyo ni kweli. Kama ni . . . wewe . . . kama hiyo ni kweli, inua mkono wako.

154 Sasa, kuna Kitu hapa ambacho unakijua. Nataka kukuuliza jambo. Katika Uwepo ambamo tumesimama sasa, na ili wasikilizaji wapate kujua, kuna hisia uliyo nayo sasa, ambayo hujawahi kuwa nayo maishani mwako. [Dada huyo anasema, "Kweli. Wala siwezi kumwelezea mtu yeyote."—Mh.] Hiyo ni kweli. Ni kwa sababu Nuru hiyo, Roho Mtakatifu yuko kati yangu na wewe; na unarudi tu, hata kwa msichana mdogo. ["Na hapo awali, nikisimama mstarini, nilihisi kama ningeninii tu . . . Nilihisi hisia ambayo siwezi kumwelezea mtu yeyote."] Wanahisi jambo lile lile, moja kwa moja mstarini hapo sasa. Mnaona? Hapa, ni katika Uwepo wa Kitu ambacho ulimwengu haujui. Njoo hapa, ili niweze kumwomba Mungu akubariki, dada.

155 Ninyi nyote, je, mnaamini kwa moyo wenu wote sasa? Mnaamini? Mnaamini? Kama mnaamini, semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

156 Baba wa Mbinguni mwenye fadhili, huyu dada yetu mpendwa amesimama hapa akiwa mhitaji. Mambo yote hufanya kazi kwa manufaa kwa wale wanaokupenda Wewe. Naye amesimama hapa, mhitaji. Naye anataka kuwa mzima. Na huu ndio wakati. Ninaomba, ya kwamba wakati huu tu, Baba, kwamba utaondoa udhaifu wake wote, mtakase kutokana na kila kitu kisicho kama Wewe. Nami ninaomba, Mungu Mpenzi, kwamba Utamsamehe kila dhambi na kosa, na kumpeleka katika Ufalme Wako, usiku wa leo, kama mtoto mchanga aliyezaliwa upya, na kuuponya mwili wake. Kupitia Jina la Yesu Kristo, Mwanao mpendwa, ninaomba. Amina.

157 Mungu akubariki, dada. Nenda, ukishangilia na mwenye furaha, Mungu akiwa pamoja nawe.

158 U hali gani, mama? Nadhani hatufahamiani, pia. Hatujuani. Lakini ikiwa—ikiwa Yesu amefufuka katika wafu, kama nisemavyo kwamba amefufuka, nami ninaamini kwamba amefufuka, Naye angekuwa amesimama hapa pamoja nasi, mimi na wewe; kisha mimi nikizungumza nawe, kama vile Yeye alivyomfanyia yule mwanamke kisimani, Naye anaweza . . . Na kwa Neno Lake aliahidi ya kwamba angefunua mambo haya, nasi tungefanya mambo yale yale aliyofanya Yeye, kwa maana angekuwa . . . Alisema, "Nitakuwa pamoja nanyi, ndani yenu, hata mwisho wa ulimwengu."

159 Sasa usitetemeshwe kwa sababu kidogo una hisia ya kigeni, lakini, hisia tukufu, lakini wewe ni, sio, huyo si ndugu yako, huyo ni Yeye, Bwana wa—wako, sio mimi, Yeye.

160 Sasa, mama huyo ni mgeni. Iweni na kicho kabisa, enyi watu; kicho kabisa, tafadhalini. Mnaona? Simjui. Mungu anamjua. Siwajui hawa watu, lakini mtajua kwamba kuna kitu hapa ambacho kinafanya kazi ya Bwana, kulingana na vile Biblia ilivyosema ingekuwa. Kama . . . Mnaamini hilo sasa? Mnaona? Vema, ni nini? Ni Bwana Yesu. Mnaona?

161 Sasa nataka tu kuzungumza naye tena, maana mimi na—namwona huyu mwanamke sasa anapoondoka kwangu. Naam, huyu mwanamke amechanganyikiwa sana kulihusu. Loo, ameharibikiwa na akili, amekuwa mahututi sana, na akashikwa na fadhaa. Bado unaugua huo. Hiyo ni kweli. Sivyo? [Dada huyo anasema, "Ndiyo."—Mh.] Iwapo ni kweli, inua mkono wako.

162 Umekuwa na hisia za kigeni sana zikipitia kwako, wakati wote. Na hasa jioni sana, unapata hisia za kigeni sana. Si ni kweli? Kisha ninakuona ukiketi kitini, kwa namna fulani jioni sana, pia. Unachoka; huwezi kufanya kazi yako. Ba—basi hiyo si ni kweli? Husababisha hata matatizo ya tumbo ndani yako, namna hiyo, asidi na kadhalika, unapokunywa kahawa au kitu kingine cha namna hiyo. Unateuka asidi, kutoka tumboni mwako, na kadhalika. Hiyo ni kweli. Ninakuona ukiondoka mezani ambapo kuna vitu kama hivyo, dirishani, karibu na dirisha. Hiyo ni kweli? Inua mkono wako kama hiyo ni kweli.

163 Sasa, Kitu fulani hapa kinajua maisha yako, sivyo? Nimewaambia, kutoka katika Biblia, ya kwamba Yesu Kristo alifanya jambo lile lile, na akaahidi ya kwamba tungefanya vile vile. Je, unaamini kuwa ni Yeye? [Dada huyo anasema, "Ndiyo."—Mh.] Ninaona uvuli mweusi kwelikweli ukikufuata, pia, ambao ni ibilisi. Naye amekujaribu nusura ujiue, siku moja, akikwambia kuwa ulikuwa—ulikuwa umevuka mstari wa kutenganisha, kwamba kamwe hutaokolewa. Hiyo ni kweli, sivyo? ["Ndiyo."]

164 Je, mnaamini, huko nje kwenye kusanyiko sasa, kwa moyo wako wote? Mnaona? Ni kamilifu. Ni kweli. Ni Bwana Yesu. Sijui maoni yenu. Najua baadhi yenu mnashangaa,

kwa sababu hamwezi kuyaficha maisha yenu sasa. Mnaona? Mnajua nisingeweza kuwafanyia chochote, lakini usingeweza—usingeweza kuyaficha maisha yako hata ufanyeje, sasa hivi. Uko Mbele Zake.

165 Sasa, dada, kama ninaweza, kwa neema ya Mungu, ninaweza kuufanya ukuache sasa. Na kama . . . Umekuwa ukishangaa, kwa wakati wa ahueni, kwa vyovyote vile. Sasa, Yeye atafanya hivyo, endapo utamwamini? Je, utamwamini? [Dada huyo anasema, "Ndiyo."—Mh.] Nitaomba. Ninyi mwaminini Yeye.

166 Sasa, angalia. Labda hujawahi kuwa karibu zaidi maishani mwako kuliko ulivyo sasa. Sasa, ili wasikilizaji wapate kujua, na rafiki yako. Mahali unaposimama sasa, hisia nyenyekevu na tamu sana imekuzunguka, (hiyo si ni kweli?) kama Kitu kilicho karibu. Si ndugu yako; lakini Kitu cha kimbinguni. Ikiwa hiyo ni kweli, inua mkono wako. Unaona? Ni Malaika wa Bwana. Unaona? Ninaishi sasa katika upeo mwingine, unaona, katika ulimwengu wa roho. Sasa nataka nikuombee wakati upako huu.

167 Sasa, Kitu chenyewe kilicho hapa, kinachoyajua maisha yako, ninakiona kikirudi nyuma kabisa kwa msichana mdogo. Ninakuona kama msichana mdogo. Ulikuwa unatoroka kitu fulani. Ni—ni kitu fulani kilichokuwa kikikufukuza. Ilikuwa ni mbwa. Ilionekana kana kwamba ulikuwa unatoka shuleni ama kitu fulani, zamani, zamani sana. Akakutisha. Umekuwa na kitu kama wasiwasi, maishani mwako mwote. Hiyo ni kweli. Sivyo? Mnaona? Wananinii tu . . . kadiri ninavyozungumza nawe, ndivyo hili ono litakavyoonyesha mengi zaidi.

Sasa, kwa ajili ya hawa wengine, na tuombe.

168 Mungu mpendwa, Mwanzilishi wa Uzima, Bwana Yesu, utakayetuhukumu sote katika Kuja Kwako; tukijua ya kwamba sisi ni watu wanaoelekea Umilele, na itabidi kukutana Nawe siku moja. Nikisimama hapa katika Uwepo Wako, na nikijua kwamba sasa hivi, hapa jukwaani, yuko Roho aliyemfufua Yesu Kristo katika wafu, na akithibitisha kila Neno.

169 Baba, Wewe unapendeza sana, kwa sababu Wewe—Wewe huyadhihirisha mambo ambayo ni ya kweli. Unaongea ukweli. Naye huyu mama amesimama hapa, ambaye anateswa na pepo mchafu ambaye anajaribu kumfanya ajiue na kufanya mambo mabaya. Lakini Wewe uko hapa kuondoa hili, Baba. Nami naomba sawasawa na Neno Lako, lililosema, "Mkimwomba Baba neno lolote katika Jina Langu, nitalifanya." Nami najua ya kwamba Neno Lako ni kweli.

170 Kwa hivyo, Shetani, wewe mwovu ambaye umemtesa dada yetu, ninakuapisha katika Jina la Yesu Kristo, Mungu aliye hai, toka ndani ya mwanamke huyu.

171 Sasa angalia upande huu. Sasa kuna jambo fulani limekupata. Unalia. Hujisikii kama ulivyojisikia, sivyo? Unajisikia mwenye furaha sasa, unajisikia vizuri. Hiyo ni

kweli? Inua mkono wako hapa, kwa watu, ili . . . Nawe unaenda, unaamini utakuwa mzima, na uende nyumbani na kumtumikia Bwana? Vema. Sasa, kimbia, uwe na furaha kweli. Hautakurudia tena.

Hebu tuseme, "Asante Mungu," huku sisi . . . Mnaona?

172 Vema, waweza kuja. Dada, nikiwa mgeni kwako, ili watu wasifikirie sasa kwamba . . .

173 Unajua "telepathia" ni nini. Hilo ndilo lililo kwenye nia ya mtu fulani. Siwezi kumtambua; na ikimtambua, nitasema wewe ni nani. Kwa hiyo, uko hapo ndani, inaendelea kunijia jukwaani. Nami nafikiri ni makasisi, maana nimeona jukwaa mbele yangu.

174 Ninataka tu uweke mkono wako kwenye wangu, dada, kama njia ya mawasiliano. Sikujui wewe. Sijawahi kukuona, na sikuangalii. Ninatazama hapa nje kwenye kusanyiko. Ikiwa Mwenyezi Mungu atanifunulia, kwa ono, ninapotazama *huku*, kilicho shida yako, ungekubali na kusema ukweli, kama ni kweli au la? Ukipenda, inua mkono wako. Sasa Bwana Yesu na atujalie ninapoomba. Ikiwa utaweka mkono wako kwenye wangu, njia tu, kama mahali pa mawasiliano. Biblia ilisema, "Kuweka mikono juu ya wagonjwa."

175 Naam, dada, una shida ya kike. Ni shida ya kina mama. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Sasa unaamini ni telepathia ya kiakili? Hiyo hufanyika. Alikuwa bafuni. Ambayo, haitakuwa sawa kuliambia kusanyiko kama hili. Huyu mama anajua ni nini; ni kuvuja. Hiyo ni kweli. Sivyo, mama? Hiyo ni kweli. Unaona? Hiyo ni kweli.

176 Sasa, Mungu pekee ndiye anayeweza kumponya. Siwezi kumponya. La hasha. Mimi si mponyaji. Mimi ni mtumishi Wake, chombo tu ambamo Roho Mtakatifu huja.

177 Kama hii papa *hapa,* hii ni spika. *Hii* si spika, hii ni bapa, mimbara. Hii ni spika; mtu fulani aliitengeneza hii kuwa spika. Mtu fulani aliifanya hii kuwa mi—mimbara. Mtu fulani alikufanya wewe mhubiri, fulani . . . Namaanisha, Bwana. Simaanishi . . . Samahani, ndugu zangu. Sikumaanisha mtu fulani alikufanya mhubiri. Sikumaanisha hivyo kwa maana hiyo, namna hiyo. Nilikuwa nasema mtu . . .

178 Na, hii, kidogo u—unafanya kazi katika sehemu mbili. Uko hapa katika ulimwengu mwingine; wakati huyo anapotoka, ndipo unaingia ndani na kuona kile kinachosimama hapa kwenye jukwaa hapa, Malaika wa Mungu, na kila kitu. Kisha unaona mambo ya kutisha yanayotendeka. Ndipo u—unashangaa wakati mwingine, ndiyo sababu nilisema . . .

179 Mungu alipokuita na kukufanya mhudumu, Mungu aliniita na kunifanya mwonaji, kama alivyoahidi katika Biblia. Biblia ilisema, "Wewe ni . . ." Nayo Biblia ilisema, kwenye . . . Katika Matendo, mlango wa pili, "Katika siku za mwisho," ndizo siku

hizi, "itakuwa kwamba nitaimwaga Roho Yangu juu ya wote wenye mwili; na vijana wenu wataona maono." Je, hiyo ni kweli? "Watatabiri." Je, hiyo ni kweli? Manabii watainuka katika siku za mwisho, na kuonyesha maono na ishara. Je, hivyo ndivyo Biblia ilivyosema? Vema, ni yale tu aliyosema Yeye.

180 Sasa, dada, nenda, ukiamini, ukiwa na imani. Amini kwa moyo wako wote, naye Mungu atakuponya. Unaamini hivyo? [Dada huyo anasema, "Ndiyo, bwana."—Mh.]

181 Baba wa Mbinguni mwenye fadhili, katika Jina la Mwanao mpendwa, Bwana Yesu, tukijua ya kwamba mwanamke huyu yuko karibu na Nuru, na kivuli moja kwa moja nyuma yake, kinachoitwa kansa. Nasi tunaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba utamjalia uponyaji wake usiku wa leo. Nami ninamhukumu adui huyu, juu ya maungamo ya imani yake, na Neno la Bwana Mungu. Ninamhukumu ibilisi huyu anayemsumbua, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

182 Nenda, furahi, dada. Usifadhaike. Amini tu kwa moyo wako wote.

183 Unataka kuponywa, sivyo, dada? Je, ungefanya... ungeniamini mimi kama nabii Wake? Kama ningekwambia mahali ilipo shida yako, na kilicho shida yako, na la kufanya, ungeamini? Ungeamini? Ingekubidi kujua kuwa imekuja kwa njia fulani. Iko mgongoni mwako, sivyo? Naam. Hiyo ni kweli. Sasa unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Una wasiwasi sana, pia, na una magonjwa ya ziada. Na mambo mengi unayoamini unayo, ambayo huna, kwa sababu ni mishipa yako, unaona, hiyo hufanya hivyo. Wakati mwingine, unapolala, unahisi kama moyo wako una shida. Lakini hicho si kitu ila tumbo lako tu. Ni kidonda kidogo kwenye tumbo lako, ambacho husababisha gesi kushinikizwa kwenye moyo wako. Haitakudhuru. Utakuwa mzima. Wewe ni mwanamke mzuri. Imani yako imekuponya. Unaniamini? [Dada huyo anasema, "Ndiyo."—Mh.] Basi nenda zako, ukishangilia, ukimshukuru Mungu.

Na tuseme, "Asante Mungu," kila mtu.

184 Dada, bila shaka, ukijua ya kwamba kitu kimoja tu ndicho kinachoweza kukuponya, hicho ni Mungu. Mungu Ndiye pekee anayeweza kuponya kansa na kukupa afya, lakini Yeye anaweza kufanya hivyo kama unaweza kuamini. Je, unaamini kwa moyo wako wote?

185 Baba wa Mbinguni mwenye fadhili, ambaye tunamwamini, naomba, Mungu mpendwa, kwamba Roho Wako mwenye nguvu zote atamgusa mwanamke huyu na kumponya. Kama ulivyosema katika Neno Lako, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Jambo la mwisho ulilosema, Yesu, ulipoliacha Kanisa Lako, ulisema, "Enendeni ulimwenguni kote mkaihubiri Injili. Aaminiye na kubatizwa ataokoka, naye asiyeamini

atahukumiwa. Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa Jina Langu watatoa pepo wachafu; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya." Bwana, Wewe ni mwaminifu kwa Neno Lako. Na juu ya agizo la Bwana Yesu, juu ya Neno Lake lenye nguvu zote, sasa ninaomba kwamba uovu huu uondoke, dada, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

186 Sasa nenda zako, mwenye furaha, ukishangilia, na uwe mzima. Amina. Ninyi nyote, ninyi kusanyiko, hamtawahi . . . Laiti ungeweza . . . Unaweza kuwazia nimerukwa na akili, lakini sijarukwa na akili. Hapana, bwana. Sijarukwa. Lakini ninasema jambo hili katika Jina la Bwana, ya kwamba Yesu Kristo Mwana wa Mungu aliyefufuka, yu hai usiku wa leo, na yuko hapa katika ukumbi huu sasa hivi, akionyesha mambo ambayo Neno Lake lilisema angefanya. Yeye si ni wa ajabu? Wa ajabu sana. Loo, jinsi alivyo mwema!

187 Nilikuwa nikimwangalia mwanamke, lakini ninaamini ni yule mama nyuma yake, ambaye ana shida ya kibofu nyongo, anayeketi kule nyuma, ambaye angetaka kuponywa. Unaamini ya kwamba Mungu angekuponya, dada? Unayeketi hapo, moja kwa moja nyuma ya huyo mama; kidogo ni mwanamke mnene anayenitazama. Naam, unaamini? Moja kwa moja nyuma ya huyo mama. Ulikuwa umeketi hapo ukiomba, sivyo? Huh? Wewe. La, huyu mama aliyeketi papa *hapa*, kuna hilo . . .

188 Laiti ungeliweza kuona, laiti ungeliweza kuona! Ni wangapi walioiona picha ya Malaika wa Bwana? Hii hapa imening'inia, papa hapa, juu ya mwanamke huyu papa hapa.

189 Anasumbuliwa na shida iliyo kwenye nyongo. Iko katika . . . moja kwa moja chini ya huu upande hapa, hiyo inasababisha matatizo. Naye alikuwa ameketi pale, akiomba dua na kuomba, Mungu amponye.

190 Dada, haitakubidi kuwa na wasiwasi tena. Kristo amekuponya. Amina. Tunamshukuru Bwana.

191 Una maoni gani, dada? Hatufahamiani. Sivyo? [Dada huyo anasema, "Hakika."—Mh.] Hatufahamiani. Yesu Kristo anatujua, sivyo? Ikiwa Mungu atanifunulia shida yako ilipo, au jambo fulani kukuhusu, ambalo unajua silijui, utamkubali kama mponyaji wako? Mimi ni ndugu yako. Ni—nisingeweza kukuponya. Mimi ni mwanamume tu, kama baba ya—yako, ama mumeo, kaka, kadhalika. Mimi—mimi si mponyaji. Lakini, unajua ya kwamba unasimama katika Uwepo Wake, au, kitu fulani, ambacho u—unajua ya kwamba kuna Kitu kilicho karibu zaidi ya mwanadamu. Hiyo si ni kweli?

192 Sasa, kwa marafiki zako huko nje, na kwa shahidi wa Bwana Yesu, wapate kujua, na ili kwamba kusanyiko liweze kuwa na uhakika. Kwa sababu, baada ya usiku huu, kutakuwa na wengi watakaosimama hukumuni. Mnaona? "Ili wapate kujua!"

193 Nataka tu kusema jambo fulani. Tangu tu uje hapa juu, hata sasa, kwamba kuna hisia halisi, nyenyekevu, nzuri, ya upendo iliyokuzunguka. Kwamba wewe. . . Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako, wala sijawahi kukuona maishani mwangu. Sasa, kwa watu wanaomjua, usingeweza kusimama karibu hivi bila kuijua, kuitambua. Naye yuko hapa. Huyo ni Roho Mtakatifu. Mnaona? Ninii. . . Ina athari kama hiyo juu ya bi—binadamu. Haina budi kuwa kitu fulani.

194 Kwa mfano, kama wewe—kama ukiona kitu kupitia jicho, kitakuwa na athari ya mhemko kwako. Na ikiwa kuna hisia ya kuhisi, na kama kitu kikiathiri hisia hiyo, ki—kinaleta mhemko, unaona. Hu—huna budi. Unaona, haina budi kutenda, nawe uko Mbele Yake. Sasa, mimi . . .

195 Kama Mungu ataniambia shida yako ni ipi, je, utamkubali Yeye kama mponyaji wako basi, kwa ajili yake? Shida yako ni tatizo la kina mama, ugonjwa wa kike. Hiyo ni kweli. Una maumivu, chini, ubavuni. Hiyo si ni kweli? [Dada huyo anasema, "Hiyo ni kweli."—Mh.] Ni mrija. Na iko kwenye-. . . Imeambukizwa. Una jipu juu yake, na linakutatiza. Wakati mwingine ni mbaya zaidi kuliko hapo awali. Ninakuona, siku kadhaa, unapojishikilia na kutembea tu, karibu tu ukisaga meno. Hiyo imekuwa hivi karibuni. Je, hiyo ni kweli? Huamini ninayasoma mawazo yako, sivyo, dada? ["Hapana."] Wewe ni mwaminio.

196 Sasa, Yesu alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Sasa, Biblia ilisema mambo haya yangetukia. Na mko sasa hivi . . .

197 Angalieni. Kwanza, Neno, Neno la Mungu lilisema ya kwamba mambo haya yangetukia.

198 Hapa, unanikaribia, mgeni, hujawahi kuniona. Na mara tu unapojongea hapa. . . Umetembea mbele ya watu wakati wote, wahudumu, lakini hujawahi kupata hisia hii maishani mwako. Unaona? Ndipo hiki hapa Kitu fulani kikishuka, Mtu huyu mzuri ambaye yuko hapa pamoja nasi sasa, anakwambia shida yako iko wapi, na yale umekuwa ukifanya. Ndipo unajua haina budi kuwa ni ya kimbinguni, sivyo?

199 Basi, unaamini kwamba mimi ni mwaminio? [Dada huyo anasema, "Amina."—Mh.] Basi nikiweka mikono juu yako, na kuombea uponyaji wako, itabidi upone, sivyo? ["Hiyo ni kweli."] Basi songa mbele, ukipenda. Naomba tu niweke mkono wangu juu ya wako.

Na tuombe, tunapoinamisha vichwa vyetu.

200 Baba yetu mpendwa wa Mbinguni, tukijua ya kwamba Uwepo Wako upo hapa, Nawe ni mwenye nguvu zote. Upo kila mahali. Nami naomba, kupitia kwa Yesu, Mwana wa Mungu, ya kwamba utamponya dada yetu. Naye amesimama

hapa Mbele Zako, sasa, Nawe unatia mafuta. Nami naomba ya kwamba umwondoe yule mwovu mwilini mwake. Sasa, tunajua ya kwamba angeyachukua maisha yake, na kumpeleka kwenye kaburi la mapema, lakini Wewe uko hapa kumwondoa. Na, Baba, tunaomba ya kwamba utafanya jambo hilo. Nasi tunajua kwamba tunapata tunayoyaomba, kwa kuwa Wewe uko hapa kutushuhudia kwamba umefufuka katika wafu. Nawe unamjua mwanamke huyu. Umemjua tangu alipokuja duniani. Nawe uko hapa ukimfunulia mambo ambayo amefanya maishani mwake, na kile kilicho shida yake.

201 Na, sasa, juu ya ma—mamlaka ya Neno la Mungu, ninakuja kumpa changamoto adui aliye mwilini mwake. Ewe adui, uitwaye ibilisi, naja, nikikiri karama niliyohudumiwa na Malaika, ambayo, Shetani, unaijua, nami nakuapisha kwa Mungu aliye hai, Yesu Kristo Mwana wa Mungu, kwamba utoke ndani ya mwanamke huyu, wala usimtese tena! Amina.

202 Mungu akubariki, dada. Nenda, ukiamini kwa moyo wako wote, utapata afya. Niandikie ushuhuda wako, uniambie ni nini kilichotokea hapa juu ulipokuja.

203 Je, ungependa kuliondokea tatizo hilo la moyo, bwana, uwe mzima? Ondoka jukwaani, useme, "Asante, Bwana Yesu, kwa kuniponya," na utapona. Amina. Amini sasa kwa moyo wako wote.

204 Nataka kukuuliza jambo fulani. Nilipomwambia "tatizo la moyo," jambo fulani lilitokea kwako. Sivyo? Maana, hilo ndilo ulilokuwa nalo, pia. Ulipokuwa umesimama kule kwenye wasikilizaji, dakika chache zilizopita, ulisema, "Ndiyo, ninaamini." Na tangu wakati uo huo, kumekuwa na tofauti ndani yako, sivyo? Hiyo ni kweli. Lakini, unaona... ["Ni—ni—ni—nilikuwa nikiwazia nilikuwa nikiamini yale uliyokuwa ukimwambia mtu yule."] Hiyo ni kweli. Hasa. ["Na hilo ni tatizo la moyo. Sikuwa nikiwazia juu ya nafsi yangu."] Najua. Lakini uliponisikia nikimwambia hivyo mtu yule, nilichosema, ndipo kitu fulani, ulijisikia kiajabu, sivyo? Sasa, hiyo ndiyo iliyokujia, kuleta uponyaji wako. Je, unaamini kwa moyo wako wote? ["Naam. Ninaamini, moyo wangu wote. Ninaamini."] Njoo, dada yangu.

205 Baba wa Mbinguni mwenye fadhili, ninaomba ya kwamba, katika Jina la Yesu, ya kwamba utadhihirisha upendo Wako kwa mwanamke huyu. Nawe utamponya na kumpa afya kabisa, ninapoweka mikono juu yake, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

206 Sasa, sijui, huko nje, ni wangapi wanaoamini sasa kwa moyo wenu wote? Mnaamini? Inua mkono wako.

207 Je, kuna mtu hapa ndani, ambaye si Mkristo, kabla hatujawaombea wagonjwa wengine zaidi, ambaye anasema, "Sasa ninamkubali Yesu kama Mwokozi wangu. Nimekuwa na hofu kidogo maishani mwangu"? Mungu akubariki, kijana

mwanamume unayeketi hapo juu. Mungu akubariki, mama unayesimama na mtoto mchanga. Mtu mwingine unaweza kuinua mkono wako, useme, "Sasa ninamkubali Yesu Kristo kama Mwokozi wangu"? Mungu akubariki, dada.

208 Kumbuka, hutawahi, pengine, hadi utakapofika Mbinguni, kuwa zaidi sana katika Uwepo Wake kuliko vile ulivyo papa hapa, ukimtazama Yeye akitembea pamoja na watu.

209 Je, mtu mwingine angeweza, tunapoinamisha vichwa vyetu kwa muda mfupi tu?

210 Baba wa Mbinguni, unataka watu wakuamini Wewe. Unataka watu wakupende. Wanne ama watano wameinua mikono yao, kwamba wanataka kukukubali Wewe kama Mwokozi wao binafsi. Ninaomba, Baba, ya kwamba utalishughulikia sasa hivi. Na jalia wanaume na wanawake, ambao bado hawajaja Kwako, ama labda wameondoka Kwako, na kuondoka kanisani, na kwenda mbali na ibada, nao wanataka kurudi Kwako, na wanajua ya kwamba Wewe uko hapa, na wao—wao wanajua kuwa ni Wewe unayezungumza nao sasa hivi, ninaomba ya kwamba kwa unyenyekevu watainua mikono yao Kwako, wakijua ya kwamba siku moja hawana budi kukutana Nawe. Na labda kabla mwaka huu haujaisha, au labda kabla juma hili halijaisha, wanaweza kuja ku—kukutana na Wewe, nao wanataka kuja katika amani, wakijua kwamba dhambi zao zimesamehewa.

211 Pia, Baba, ninawapa, kwa Neno Lako, ahadi; kwamba ulisema, "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele; na hataingia hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani."

212 Wakati tumeinamisha vichwa vyetu, na muziki unachezwa, sijui, rafiki Mkristo, ama rafiki mwenye dhambi, kuna mwingine humu ndani? Si kwangu, ndugu yako; lakini kujua kwamba Bwana Yesu yu karibu, je, waweza kuinua mkono wako? Huku vichwa vyenu vimeinamishwa, mtu asiangalie, tafadhali. Inua tu—inua tu mkono wako kwa Mungu, na kusema, "Kwa mkono huu ulioinuliwa, sasa nataka kumpokea Yesu kama Mwokozi wangu. Wakati akiwa karibu nami hivi, ninataka kumkubali kama Mwokozi wangu." Je, mwaweza kuinua mikono yenu? Mungu akubariki; wewe; wewe hapo chini, msichana; wewe, mvulana mdogo; wewe, msichana; na wewe. Hilo ni zuri. Mungu akubariki. Bwana Yesu na awarehemu, kila mmoja.

213 Je, kuna wengine hapa ambao walikuwa wakienda kanisani na kushiriki katika kanisa fulani mahali fulani, nawe ukaliacha tu kanisa, huendi kanisani tena? Sijali ni kanisa gani; hilo halijalishi. Lakini unataka kurudi kanisani mwako, na kuchukua ushirika wako tena pamoja na watoto wa Mungu, nawe unataka kukumbukwa katika maombi, kwamba Mungu akuruhusu kurudi? Inua mkono wako. Je, utafanya hivyo? Mungu

akubariki. Loo, jamani! Kuna mikono dazani moja, nadhani, iliyoinuliwa. Sasa, hilo ni zuri sana. Fanya hivyo, sivyo?

214 Ndugu yetu, mchungaji, atawaita madhabahuni, baada ya muda kidogo, ndugu, Junior Jackson, kwa ajili ya wito huu wa madhabahuni, katika muda mfupi tu.

215 Lakini nataka kukuuliza swali. Je, unaamini sasa kwamba Bwana Yesu yuko hapa, nawe ungetaka kuponywa? Je, utainua mkono wako, uinue tu mikono yako kama unataka kuponywa? Mungu akubariki. Mungu akubariki.

Sasa huku mmeviinamisha vichwa vyenu.

216 Ninamwona mama mmoja ameketi papa hapa, hebu kidogo. Naam, ana ugonjwa wa kike. Anayeketi papa hapa, ameinua mkono wake kuelekea kichwani mwake. Mungu akubariki, dada. Mkono wako uliinuliwa dakika chache zilizopita. Huna haja ya kuwa na wasiwasi tena. Mungu, anakuponya; imani yako.

217 Ndugu, wewe unayeketi hapo nyuma ukinitazama, kwa kutetemeka, kwa namna fulani ya kupooza, una ugonjwa wa tezi kibofu. Inakubidi kuamka usiku. Sivyo? Hiyo ni kweli. Naam, bwana. Na sasa, kwamba, unaamini ya kwamba Yesu Kristo anakuponya? Kama unaamini, vema, basi unaweza kupokea uponyaji wako. Mungu akubariki. Hilo ni sawa.

Sasa iweni na kicho kweli, kila mtu.

218 Juu kwenye roshani hapa, mkono wangu wa kulia, mtu fulani hapo aseme, "Bwana Mungu, ninakuamini kwa moyo wangu wote. Ninataka kukumbukwa katika maombi sasa hivi." Je, unaweza kuinua mkono wako, haidhuru umetoka wapi. Mungu akubariki, mwanangu. Mungu akubariki, dada. Mungu akubariki. Mungu akubariki.

219 Ninaona maji, yakitiririka. Ni mmishenari ameketi hapa akiomba, pia. Bwana Mungu akubariki, dada yangu, na akupe shauku ya moyo wako, pia. Bwana awe pamoja nawe.

Wasema, "Unajuaje jambo hilo, Ndugu Branham?"

Sina budi kulisema. Huyu hapa, Malaika wa Bwana yupo.

220 Sasa, wewe, nitakuomba ufanye jambo fulani. Wewe ambaye umeketi karibu na mtu fulani, ambaye ni mgonjwa, waweza kuweka mikono yako juu yao kwa muda kidogo tu, kwa maombi, mwekeane mikono mmoja kwa mwingine, kwa ajili ya maombi? Hiyo ni kweli. Mungu atasikia maombi yenu pia. Anawapenda. Yeye yuko hapa, naye anataka kukuponya.

221 Baba yetu wa Mbinguni, ninalileta kusanyiko hili Kwako sasa hivi, nikijua ya kwamba Wewe uko hapa, hujashindwa hata kwa kimoja. Hushindwi kamwe, Bwana. Wewe ni Mungu, na huwezi kushindwa. Na mtazamo Wako kwa watu hawa kumi ama kumi na watano wanaokuja jukwaani, usiku wa leo, ndio mtazamo Wako kwa kila mmoja. Kadhaa huko kwenye

kusanyiko, labda wanane au kumi kwenye kusanyiko kule, ambao umeonyesha maono juu yao, ukawaambia magonjwa yao yalikuwa yapi, na yalivyokuwa. Mbona, Wewe ni Bwana Yesu. Unawajua wote. Na Unaweza kufunua, kwa watumishi Wako wanyenyekevu, yale ambayo yanahitajika.

222 Nami naomba, Baba wa Mbinguni, sasa hivi, ya kwamba Wewe uwaone, kama walivyo sasa. . . Nami ninaomba kwamba juu ya moyo Wako mkuu, ambao najua umezidi sana yale huruma ya kibinadamu ingekuwa, lakini Wewe waangalie na kuona haja zao, na kumponya kila mmoja. Bwana, unajua hali zao. Nami naomba, kupitia Jina la Yesu, ya kwamba, sasa hivi, ya kwamba utawaponya.

223 Naye adui, ibilisi ambaye amewafunga, na kutokuamini ambako kumewafunga kwa hali, ninakuapisha, ewe adui wa Yesu Kristo, kwamba utoke ndani ya watu hawa, na uwaache, kupitia Jina la Yesu Kristo.

224 Sasa, huku vichwa vyenu vimeinamishwa, mkiamini kwa moyo wenu wote, ya kwamba Yesu Kristo Mwana wa Mungu yuko hapa, na akiwapa afya, kwamba mmeketi Mbele Zake, nanyi mnaamini. Na kama unaamini kwa moyo wako wote, na kuamini ya kwamba unaweza kukubali uponyaji wako, huku umeinamisha kichwa chako, inua mkono wako; kama unahisi unaweza kukubali uponyaji wako, ya kwamba umeponywa. Mungu awabariki. Hiyo ni ajabu. Kusanyiko lote, na kila mmoja, naamini, aliyeinua mkono wake, sasa wanakubali uponyaji wao. Bwana awabariki.

225 Tunapoinamisha vichwa vyetu tena, kwa ajili ya maombi kutoka kwa Ndugu Junior Jackson, huku vichwa vyenu vimeinamishwa. Vema, Ndugu Jackson, Bwana. . . [Ndugu Jackson anaomba—Mh.]

56-0200 Kuishindania Ile Imani
Georgetown High School
Georgetown, Indiana Marekani

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org